


UKURASA 3



## RC Mtaka aagiza sensa ifanyike usiku, mchana




UKURASA 9

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumapili Agosti 28, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
JUMAPILI
ISSN 0856 • No. 0581051
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Mbuyu ulivyoua wapenzi kikatili

**MAJIRANI** wasimulia waliyoshuhudia...

*Endelea ukurasa 2*



Mti wa mbuyu ukiwa umeangukia nyumba yenye vyumba vitano, Mkunguni A, Kinondoni Mkwajuni mkoani Dar es Salaam juzi usiku na kusababisha vifo vya watu wawili. **PICHA: ROMANA MALLYA**

# Mchimbaji mdogo anasa jiwe la tanzanite la bil. 2/-

UKURASA 5




Bilionea mpya wa madini ya tanzanite, Anselim Kawishe (katikati), akiwa ameshika madini yake yenye thamani ya Sh. bilioni 2.245 Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara jana. Kulia ni Waziri wa Madini, Dotto Biteko na (kushoto) ni Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Florens Luoga. **PICHA: GIFT THADEY**

UKURASA WA 3

## DC ANUSA WIZI WA DAWA

MKUU wa Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza, Hassan Masala, amenusa harufu ya wizi wa dawa za serikali katika hospitali mbalimbali za umma na kuzipeleka kwenye maduka binafsi ya dawa kwa ajili ya...

## Shehena mahindi yazuiwa mpakani

UKURASA 2

MICHEZO SIMBA SC YAKATAA KUMWACHIA ONYANGO UK. 24
MAONI, KATUNI UK.6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikabidhiwa Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2020/2021 na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Othman Abass Ali, Ikulu jijini Zanzibar jana. Kulia ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar, Haroun Ali Suleiman. **PICHA: IKULU**

# Mbuyu ulivyoua wapenzi kikatili

**Na Romana Mallya**

WATU wawili ambao ni wapenzi wamefariki dunia baada ya tawi kubwa la mbuyu kukatika na kuiangukia nyumba yenye vyumba vitano waliyokuwa wamelala eneo la Mkwajuni wilayani Kinondoni mkoani Dar es Salaam usiku wa kuamkia jana.

Waliofariki ni mama lishe, Asha Baruani (36) na kijana ambaye majirani walidai hawamfahamu kwa jina na kwamba juzi jioni walimwona kwa mara ya kwanza akifika kwa jirani yao huyo na saa chache kukumbwa na baa hilo.

Tukio hilo la kusikitisha lilitokea majira ya 5:30 usiku kwenye nyumba hiyo iliyoko kwenye kingo za Bonde la Mto Msimbazi, pembeni mwa Barabara ya Kawawa.

Nyumba hiyo iko mita chache kutoka Kituo cha Daladala cha Mkwajuni kuelekea Magomeni, ikiwa ni miongoni mwa nyumba chache zilizosalia baada ya bomoabomoa iliyowakumba watu waliokuwa wanaishi bondeni mkoani Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana eneo la tukio, Hamida Mtilwa, mmiliki wa nyumba hiyo ambayo Asha alikuwa mpangaji wake katika chumba kilichoangukiwa na tawi la mbuyu, alisema tukio hilo lilitokea wakati ambao wote walikuwa wamelala.

"Nyumba hii ina vyumba vitano, tuliokuwa ndani ni watu watano yaani mimi, mtoto wangu mwenye umri wa miaka 13 ambaye anasoma darasa la saba, kaka yangu ambaye alikuja kunitembelea na mpangaji wangu, Asha na mpenzi wake," alisimulia.

'Mama mwenye nyumba' huyo (Hamida) alisema kuwa akiwa chumbani kwake, ghafla alishtuka baada ya kusikia kishindo kikubwa na alipoamka, aliona bati la chumba chake likiwa limetumbukia ndani na matofali yamebomoka.

"Nilipokwenda nje, nikakuta mbuyu umeshadondoka, umeangukia chumba cha mpangaji wangu Asha ambaye ndani alikuwa amelala na mpenzi wake ambaye alinitambulisha jana (juzi) jioni baada ya kuja naye hapa kuwa ni mpenzi wake, huyu kijana simfahamu, ni mara yake ya kwanza kuja hapa," alisimulia.

Aliendelea kubainisha kuwa Asha amekaa kwenye nyumba hiyo kama mpangaji kwa karibu miezi mitano na alikuwa akilipa Sh. 25,000 kodi ya chumba kwa mwezi.

"Huyu mwanaume ninaona watakuwa wanalingana, siyo mkubwa sana, tunaiomba serikali itusaidie kwa sababu mti huu umedondoka sehemu na mwingine umebaki (matawi mawili yamebaki), waje kuukata wote ili usiendelee kuleta maafa kwa sababu kama unavyoona hapa, kuna nyumba zaidi ya tatu zimeuzunguka huu mbuyu," alisema huku akionyesha mazingira yaliyoko huko.

Hamida alisema katika tukio hilo, chumba kimoja kimebomoka kabisa na vingine vilivyobaki ambavyo ni vinne, vimeathiriwa kwa kiasi kikubwa na mti huo.

"Nimeambiwa na viongozi waliofika hapa leo (jana) asubuhi kwa ajili ya usalama wetu tusilale humu ndani, kama unavyoona mwenyewe baadhi ya vyumba matofali yameanguka, mtoto wangu amepata michubuko mwilini," alisema.

Hamida alibainisha kuwa mpaka wakati huo, kitu pekee ambacho alikuwa ameokoa ni yeye na mwanawe lakini vitu vingine vyote vipo ndani ya nyumba hiyo na wamelazimika kuweka ulinzi nje ya nyumba hiyo.

"Ninawaomba Watanzania wenzangu kutokana na changamoto iliyonipata na kwa sasa sina pa kulala na mtoto wangu, na mimi shughuli zangu kubwa ni uokotaji wa chupa mtaani, ninaomba msaada wa fedha za kujikimu kwa kipindi hiki kigumu ninachopitia," Hamida aliomba msaada na kutaja namba zake za simu ambazo ni 0659 627434.

Shuhuda wa tukio hilo, William Laurence anayeishi jirani na nyumba hiyo iliyoangukiwa na tawi la mbuyu, alisema kuwa juzi jioni akiwa ameketi chini ya mti huo, Asha alifika huko akitokea kwenye mihangaiko yake.

"Tulikaa hapo mpaka saa moja hivi usiku, akashuka huku chini (eneo la Bonde la Mto Msimbazi), akawa anaongea na vijana waliokuwapo wakati huo, baadaye akapandisha juu na kurudi na kijana (marehemu) ambaye ndiyo kwa mara ya kwanza ninamwona, akanitambulisha kuwa ni mpenzi wake.

"Akamtambulisha na mama mwenye nyumba wake (Hamida) kuwa 'huyu ni mume wangu', basi baadaye nikaondoka kwenda nyumbani na mama mwenye nyumba alikuja akaangalia TV nyumbani kwetu, baadaye akaondoka kwenda kulala.

"Nikiwa ndani, nikawa ninaona kama ardhi inatikisika na nje nikawa ninasikia kishindo, nikajua labda gari limefeli breki," alisimulia.

Laurence alisema wakati anatoka ndani kwake kwenda nje kushuhudia alichokihisi, alikutana na dada yake mlangoni akamrudisha ndani na kumwambia mti unadondoka.

"Baada ya mti kuanguka tulipokuja hapa tukakuta chumba cha mpangaji ndiyo kimedondokewa na mti, tukaanza kuwatafuta kwenye kifusi cha nyumba na kumkuta Asha na huyo kijana wakiwa kwenye godoro lakini mwanamke alikuwa bado hajafa, ila yule mwanamume alikuwa ameshafariki dunia.

"Kaka wa mama mwenye nyumba akafanya utaratibu akamchukua Asha na kumpeleka Hospitali ya Magomeni na baadaye Hospitali ya Mwananyamala, alitupigia simu kuwa amefariki dunia, polisi walifika wakauchukua mwili wa yule kijana na kuupeleka Mwananyamala," alisema.

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Kinondoni Mkwajuni Mkunguni A, Rashid Seleman, alisema kuwa baada ya tukio hilo, waliomba msaada polisi ambao walifika usiku huo na kuchukua mwili.

Alisema Mbunge wa Kinondoni, Abbas Tarimba, pia alifika eneo hilo na kuwaeleza kuwa kwa sababu sehemu ya mti huo bado haijadondoka, waangalie uwezekano wa kukatwa.

"Wamekuja wataalamu wa misitu hapa kuangalia namna ya kuuondoa, wamesema wapo tayari muda wowote kuuondoa lakini changamoto ikaja kuna nyumba kama mbili zitaathirika wakati wa kuuondoa, kuna nyumba moja ina chumba na choo na nyingine yenye vyumba vitatu," alisema.

Katibu wa Afya Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwananyamala, Rajabu Kaseke, alipotafutwa na Nipashe jana, alikiri kupokea miili ya watu hao, akiwa na ufafanuzi kwamba wote wawili walipokewa hospitalini huko jana wakiwa ni wafu.

Katika ufafanuzi wake kwa Nipashe, Kaseke alisema miili iliyopokewa ni ya Asha Baruani (36) na dereva Charles Nelson (36), yote imetambuliwa na ndugu zao.

# Malori yenye shehena ya mahindi yazuiwa mpakani

**Na Samson Chacha,** TARIME

MALORI zaidi ya 100 yenye shehena ya mahindi yaliyokuwa yakisafirisha kwenda Kenya kupitia Mpaka wa Sirari wilayani Tarime mkoani Mara, yamekwama kwa wiki moja sasa kutokana na wafanyabiashara waliokuwa wanayasafirisha kuwa na vibali vilivyokwisha muda wake.

Wakizungumza na waandishi wa habari juzi katika mpaka huo, baadhi ya madereva wa malori hayo waliojitambulisha kwa majina ya Said Omar, Swalehe Juma, John Masalu, Kimario Masawe, Joseph Alois na Sobe Marwa, walidai kukwama mpakani huko kwa wiki moja sasa.

"Haya malori unayoyaona kila kona ya Mji wa Sirari na vitongoji vyake yakiwa na shehena ya magunia ya mahindi, tumekwama hapa Sirari kwa wiki moja sasa.

"Tulikuwa tunasafirisha magunia haya ya mahindi kwenda Kenya, baadhi ya shehena za mahindi tumetoa Tunduma. Wafanyabiashara wenye shehena hizi waliokuwa na leseni na vibali vya kusafirisha nafaka kwenda nje ya nchi, vibali vyao vimekwisha muda, hali iliyochangia kukwama hapa," alidai Said Omar, mmoja wa madereva hao.

Madereva hao waliwaomba mabosi wao, wafanyabiashara wenye shehena hiyo, kufanya jitihada za kupata vibali vya kusafirisha nafaka ili wavipeleke walikokusudia, baadhi wakilalamika kuishiwa fedha kwa ajili ya matumizi.

Ofisa Kilimo Kituo cha Forodha Sirari, Philipo Lustola, alipoulizwa na Nipashe kuhusu kukwama kwa malori hayo, baadhi yakiwa ndani ya uzio na mengine nje ya kituo chao yameegeshwa, alisema:

"Malalamiko ya madereva hao tuliyapata na Alhamisi, tuliwaita tukafanya nao kikao cha pamoja ambapo tatizo kubwa ni wafanyabiashara wenye nafaka hizo hawana leseni na vibali vya kusafirisha nafaka nje ya nchi.

"Vibali vilivyokuwapo vimekwisha muda wake na nafaka walizotakiwa kusafirisha nje ya nchi walishasafirisha kupitia kituo hiki. Tunakwenda na takwimu kulingana na vibali vilivyotolewa, hatuzuii wafanyabiashara kusafirisha nafaka nje ya nchi bali tunawashauri kuwa na nyaraka halali na vibali vinavyoonyesha idadi ya tani wanazotakiwa kusafirisha kwenda nje ya nchi.

"Baadhi ya wafanyabiashara wenye nafaka walisema kuwa huenda vibali vikaanza kutoka Jumatatu wiki ijayo. Tunatoa wito kwa wafanyabiashara hao kutopitisha nafaka kupitia njia za panya kwenda nje ya nchi kwani kufanya hivyo ni kinyume cha taratibu na kuvunja sheria za nchi.

"Wanatakiwa kuwa na subira ili wapate vibali na kupitisha katika ofisi za serikali ili kupata takwimu sahihi za nafaka zinazonunuliwa."

## HABARI KITAIFA

# Ataka makarani wa sensa wafanye kazi usiku, mchana

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe amewataka makarani wa sensa mkoani mwake wafanye kazi usiku na mchana ili wananchi wote wahesabiwe.

Antony Mtaka alitoa agizo hilo jana akiwa Kijiji cha Ilunda, Kata ya Mtwango wilayani Njombe wakati akikagua utekelezaji wa sensa.

Alisema wananchi wa Mkoa wa Njombe ni watu wanaofanya kazi kwa bidii, wakitoka nyumbani asubuhi na kurejea jioni, hivyo baadhi yao walifika kwenye ofisi za serikali kuomba muda wa ziada ili kuwawezesha kuhesabiwa.

Alisema kwa kuliona hilo na kushirikiana na Jeshi la Polisi, maeneo ambayo yataonekana kuwa na uhitaji mkubwa wa watu kutaka kuhesabiwa muda wa jioni kutokana na kubanwa na majukumu, jeshi hilo litasaidia kwenye suala la ulinzi na usalama.

"Kwenye mtaa husika kutakuwa na gari la doria ambalo litakuwa linapita kwa wakati wote ambao maofisa wa sensa watakuwa wanafanya kazi hiyo kwenye muda wa ziada ambao ni saa moja hadi saa mbili usiku," alisema.

Mtaka alisema lengo la kuweka doria ni kuweka ulinzi ili wasitokee watu wengine ambao siyo makarani wa sensa wakatumia nafasi hiyo kufanya uhalifu.

Aliwataka makarani wa sensa mkoani hapo kuacha kuhesabu watu ndani ya nyumba zao, vinginevyo mhusika awe na matatizo ya kiafya au mgonjwa.

"Kama mtu hana matatizo yoyote, ni mzima, kivuli cha nje ya nyumba kitumike kuhesabu watu na siyo vinginevyo," Mtaka aliagiza.

Baadhi ya makarani wa sensa kwenye maeneo mbalimbali mkoani hapo, wakiwamo Tukopasya Mwaipopo na Grecious Chembela, walisema wananchi walio wengi ni waelewa na wanakubali kuhesabiwa ingawa wapo wachache ambao wamekuwa wakigoma kutokana na sababu mbalimbali.

"Kuna mzee alionyesha utata wa kugoma kuhesabiwa kwa kile alichodai kuwa kuna mambo ya kifamilia yameleta mgogoro na ameshindwa kusaidiwa," alisema Chembela.

Mkazi wa Kijiji cha Ilunda ambaye awali aligoma kuhesabiwa, Severine Kaduma, alisema sababu ya kugoma kuhesabiwa ni kudhulumiwa mali za marehemu baba yake licha ya kufuatilia suala hilo kwa viongozi wa ngazi mbalimbali.

"Ni kweli nilifanya mgomo wasiniandikishe kwa kuwa walishindwa kunitekelezea mambo yangu lakini baada ya kuongea na mkuu wa mkoa, sasa nipo tayari," alisema Kaduma.

# Mkuu wa Wilaya anusa wizi wa dawa

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKUU wa Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza, Hassan Masala, amenusa harufu ya wizi wa dawa za serikali katika hospitali mbalimbali za umma na kuzipeleka kwenye maduka binafsi ya dawa kwa ajili ya kuuzwa kinyume cha sheria.

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani wilayani humo juzi, Masala alisema baadhi ya watumishi wa umma katika vituo vya afya wamekuwa wakiiba dawa na kuziuza kwa watu binafsi.

Alitoa mfano kuwa hivi karibuni kuna dawa zilitolewa Kituo cha Afya Sangabuye kwenda Kituo cha Afya Buzuruga lakini hazikufika na kwamba ufuatiliaji umebaini ziliibwa na kuuzwa kwenye maduka binafsi.

"Kuna upotevu wa dawa katika Kituo cha Afya Sangabuye na baadhi ya waliofanya hivyo wanajulikana na walichukua dawa hizo wakidai kuzipeleka katika Kituo cha Afya Buzuruga ambako hazikufikishwa," alisema.

Alibainisha kuwa baada ya uchunguzi kufanyika, imegundulika dawa hizo zipelekwa kwenye vituo vya afya binafsi vilivyofunguliwa na watumishi hao wa serikali. Alisema serikali wilayani humo imewavumilia vya kutosha watumishi kama hao na sasa haiko tayari kubeba mtu ambaye anahujumu mali za serikali na kuwakosesha huduma muhimu wananchi.

Alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ilemela, Modest Joseph, kuchukulia hatua za kisheria dhidi ya watumishi hao kwa kuwa kuna ushahidi dhidi yao.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa wizi huo ulifanyika katika Kituo cha Afya Sangabuye na ofisi yake imechukua hatua za awali dhidi ya watumishi hao.

"Huo wizi uliotokea Januari tayari tumekwishachukua hatua na pia kuna huu uliotokea Agosti 2, mwaka huu, katika Kituo cha Afya Sangabuye na watumishi hao tumewachukulia hatua za awali na hatutasita kuwachukulia hatua zingine zaidi ikiwamo kuwafikisha mahakamani.

Katika hatua nyingine, Baraza la Madiwani wilayani Tarime mkoani Mara limewafukuza kazi watumishi wawili wa halmashauri hiyo kutokana makosa ya utoro kazini kwa zaidi ya miezi sita.

Baraza hilo pia limemsamehe mtumishi mmoja aliyekuwa mtoro kazini baada ya kuomba radhi na kueleza sababu zilizomfanya asiwapo kazini huku likiagiza mtumishi mwingine aliyeondolewa kazini kutokana na kubainika kuwa na vyeti vya kughushi, suala lake lijadiliwe.

Akizungumza katika kikao cha baraza hilo juzi, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Daniel Kamote, alisema watumishi waliofukuzwa kazi walitoroka kazini kwa zaidi ya miezi sita.

Alimtaja mtumishi wa kwanza aliyefukuzwa kazi kuwa ni Ali Salum ambaye ni tabibu, ikiwa ni takriban miezi sita haijulikani aliko.

Mtumishi mwingine ni Doris Akoko ambaye ni muuguzi, pia hayuko kazini kwa miezi sita na hawana taarifa zake.



Diwani wa Kata ya Kivukoni, Sharik Shoughule (kushoto), akichangia damu wakati wa upimaji wa afya bure, ulioandaliwa na Jumuiya ya Khoja Shia Ithna Asher Jamaat, kama kumbukizi ya kifo cha mjukuu wa Mtume Muhammad (S.A.W), Imam Hussein, katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mkoa wakabidhiwa magari matano kwa ajili ya sensa

**Na Restuta Damiana,** BUKOBA

MKOA wa Kagera umepokea magari matano kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa ajili ya kusaidia shughuli za sensa inayoendelea nchi nzima.

Akizungumza baada ya kupokea magari hayo juzi, Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, alisema serikali kwa kutambua umuhimu na kuona uhitaji wa magari katika mkoa huo, imeamua kuwasaidia ili kuhakikisha kazi hiyo inafanyika kwa ufanisi.

Chalamila alisema magari hayo yatapelekwa katika wilaya mbalimbali kwa lengo la kurahisisha shughuli za ufuatiliaji wa kazi ya sensa.

"Tumeomba magari haya ili sensa isikwame inapotokea shida katika halmashauri nane na wilaya saba za mkoa huu ili tuzitatue na kupata takwimu sahihi za sensa kwa maendeleo endelevu," alisema.

Chalamila alisema kuwa kuanzia Agosti 23 mwaka huu, wananchi wamekuwa na mwitikio mzuri kuhusu kuhesabiwa licha ya baadhi yao kutoa maneno yenye mzaha. Aliongeza kuwa kazi hiyo ya sensa ina manufaa kwa taifa kwa kuwa serikali itapata takwimu sahihi na kufanya maendeleo ikiwamo ujenzi wa stendi ya kisasa ya mabasi mjini Bukoba.

Katika hatua nyingine, Chalamila ameitaka Tume ya Ushindani (FCC) kushirikiana na vyama vya ushirika ili kuendeleza zao la kahawa. Katika kikao cha wadau wa kilimo na ushirika mkoani humo juzi, Chalamila alisema kuwa moja ya majukumu ya FCC ni kumlinda mlaji, hivyo kuna haja kahawa inayozalishwa mkoani humo iwe bora.

"Kukiwa na mabadiliko ya taarifa ni sehemu ya kumlinda mtumiaji na ukiangalia mfumo wa Tume ni Ushindani na majukumu ya vyama vya ushirika ni kumlinda mkulima, lazima vishirikiane kuleta tija na kulinda zao hilo kwa mkulima," alisema Chalamila.

Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani Kagera, Robert John, alisema vyama hivyo vipo kwa ajili ya kuhakikisha wakulima wanazalisha kwa tija na kutetea maslahi yao.

Mwakilishi wa FCC, Magdalena Utouh, alisema kuna athari za uuzaji wa bidhaa bandia ambazo humfikia mlaji, mojawapo kumwondoa katika soko mfanyabiashara wa bidhaa halisi kwa kuwa bidhaa bandia huuzwa kwa bei ya chini.


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**JASTIN JACOBO NNKO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya SUZUKI yenye usajili namba **T191 AFQ.** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/339269/2022**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKE Kituo cha JUMUISHI Mkoa D'SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi Na..1596/ 2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU PILLI ALLY MAZENGO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MIRAJI ATHUMANI ULIZA**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 12 mwezi 09 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

**Zingatia;**

Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta makamani kukaguliwa.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na wawezza kukaguliwa.

Marehemu hakuacha wosia

Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 25 mwezi 08 mwaka 2022

HAKIMU



**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**MANFRED X ROTHBLETZ** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T354 AQG**, CHASSIS NAMBA **:SX906506833.** KWA YEYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/334479/2022**

# RC ajivunia kwa mafanikio sensa

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, amesema takwimu ya kitaifa ya sensa zinaonesha hadi kufikia Agosti 26, mwaka huu, saa moja asubuhi, Mkoa wa Ruvuma ulikuwa umefikia asilimia 63 ya lengo la kuhesabu zaidi ya kaya 450,000.

Kanali Thomas alibainisha hayo alipozungumza na wananchi wa Peramiho, nje kidogo ya Mji wa Songea, alipozuru kukagua maendeleo ya Sensa ya Watu na Makazi inayoendelea nchini nzima.

Alisema kutokana na takwimu hizo za kitaifa, mkoa huo unakwenda vizuri, akitoa rai kwa wananchi kuendelea kushirikiana na makarani kwa kujitokeza kuhesabiwa ili kupata takwimu sahihi za idadi ya watu na makazi itakayoisaidia serikali kupanga mipango ya maendeleo.

Kanali Thomas alisema anatamani Mkoa wa Ruvuma uvunje rekodi za kitaifa kwenye majumuisho ya sensa kwa kuongoza kitaifa katika utekelezaji wa kazi hiyo.

Aliwapongeza watendaji kwa usimamizi mzuri katika sensa, akiwataka viongozi wa halmashauri zote kuendelea kuwaelimisha wananchi wajitokeze kuhesabiwa ili kufikia malengo ya mkoa na taifa kwa ujumla.

"Matumaini yangu tunakwenda vizuri, niwaombe wananchi wenzangu endeleeni kujitokeza ili tupate takwimu sahihi, data hizi zina manufaa kwetu na kwa taifa letu," alihimiza.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Neema Maghembe, alisema halmashauri hiyo yenye kata 16, inatarajia kuhesabu kaya zaidi ya 36,000 na kwamba hadi kufikia Agosti 25 mwaka huu, wamefanikiwa kuhesabu zaidi ya kaya 28,000.

"Nikuhakikishie mkuu wa mkoa, kazi hii inakwenda vizuri na watu wanajitokeza kuhesabiwa, hata kaya ziliotembelea umekuta kazi inakwenda vizuri," alisema.

Sensa ya Watu na Mkazi ilianza rasmi kitaifa Agosti 23, mwaka huu na inatarajiwa kukamilika baada ya siku saba tangu kuanza kwake. Sensa hii ni ya saba kufanyika tangu uhuru wa nchi.

# Machinga wanavyorejea kwa kasi katikati ya jiji

**Na Pelusy Yohana** (SAUT)

BAADHI ya wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga, wameanza kurejea kwa kasi katika maeneo ya katikati ya Jiji la Mwanza, wakizikimbia sehemu walizopelekwa na serikali kwa ajili ya kufanyia shughuli zao.

Wakizungumza na Nipashe juzi, wafanyabiashara hao walisema baadhi yao wanalazimika kurudi katikati ya jiji kwa kuwa sehemu walizopelekwa hazina wateja.

Waliomba maeneo hayo kuwekwa vituo vya daladala zinazoshusha na kupakia ili kuwavutia wateja kufika na kununua bidhaa zao.

"Tuna shida katika kupata wateja katika maeneo yetu haya mpaka baadhi machinga wamekuwa wakikimbia maeneo haya kutokana na kutokuwapo kwa wateja kama ilivyokuwa katika maeneo ya awali yaliyokuwa na stendi," alisema Isaya Lukas, mmoja wa machinga.

Isaya ambaye anafanya biashara katika Soko la Mchafukoga lililoko Igogo jijini Mwanza, alisema katika soko lao miundombinu yake siyo rafiki kwa biashara zao, hivyo akaiomba serikali kutatua kero hiyo ili wabaki katika maeneo hayo.

Neema Joseph, mmoja wa machinga, alisema hali ngumu ya mzunguko wa fedha katika maeneo hayo ndiyo inasababisha baadhi yao kukimbia na kurudi kupanga biashara barabarani na mbele ya maduka ya watu.

Alisema machinga wengi hawauzi bidhaa zao kama walivyokuwa kwenye maeneo ya katikati ya jiji kwa kuwa huko waliko sasa wateja ni wachache. Mwenyekiti wa Wafanyabiashara hao, Magaiga Mtatiro, aliiomba serikali kutatua kero ya kukosekana stendi maalum ya kupakia na kushusha abiria.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuchangamsha biashara zao huku akiwaomba wafanyabiashara kuendelea kubaki katika maeneo hayo ili yazoeleke kwa wateja.

"Tunaishukuru serikali kwa kutupanga katika maeneo haya, tunaomba kutatuliwa kero za miundombinu ili tufanye kazi kwa amani katika maeneo haya.

"Vilevile, niwasihi wafanyabiashara wenzangu wanaorudi barabarani, kuacha kabisa na kubaki katika maeneo tuliyopangiwa ili wateja wayazoee," alisema.

Tangu Halmashauri ya Jiji la Mwanza iwapangie machinga maeneo maalum ya kufanyia biashara, baadhi yao wamekuwa wakikaidi na kurudi kupanga bidhaa zao katikati ya jiji hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana mkoani Mwanza, Amiana Makilagi, alipotafutwa na Nipashe kuzungumzia suala hilo, alisema kwa sasa hawatasumbuka na wafanyabiashara hao badala yake wakiwakamata watawafikisha mahakamani.

"Kwa sasa hatutasumbuka na machinga kwa kuwa tayari Jiji la Mwanza limetunga sheria ndogo ambazo tutazitumia kuwafikisha mahakamani," alionya.



Waumini wa Kanisa Katoliki Parokia ya Kristo Mfufuka, wilayani Muheza, mkoani Tanga, wakimlaki Padri Martin Kihiyo (juu ya gari), aliposwasili katika parokia hiyo, kwa ajili ya sherehe maalum ya Jubilei ya kutimiza miaka 25 ya upadri wake, jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Waziri ataka uhusiano mzuri hifadhi, wananchi

**Na Mwandishi Wetu,**
SENGEREMA

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, amewataka wahifadhi kujenga uhusiano mzuri na wananchi wanaoishi pembezoni mwa hifadhi ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yao ya kuhifadhi rasilimali za taifa.

Alitoa rai hiyo jana alipofanya ziara ya kikazi katika Shamba la Miti Buhindu wilayani Sengerema mkoani Mwanza.

"Jengeni uhusiano mzuri na jamii na zinapokuwa na mahitaji ambayo yako ndani ya uwezo wenu, msisite kuwasaidia," aliagiza.

Alisema uwapo wa uhusiano mzuri utasaidia kupunguza tatizo la uchomaji wa mkaa, wizi wa miti, uingizaji mifugo ndani ya hifadhi na majanga ya moto kwenye misitu.

Pia aliwataka wahifadhi kuweka utaratibu mzuri wa uvunaji wa miti kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo iliyoKo.

"Tengenezeni mazingira rafiki ya utaratibu ulio wazi wa uvunaji miti, kila mtu aingie kwenye ushindani bila kumwonea mtu," aliagiza.

Meneja wa Shamba la Miti Buhindi, Mussa Tinda, alisema shamba hilo limekuwa likisaidia jamii katika nyanja mbalimbali ambapo Sh. milioni 150 zimetumika.

"Tumetoa mifuko ya simenti 300 kwa Kata ya Kafunzo, ujenzi wa mabweni na vyumba vya madarasa, uchimbaji wa kisima cha maji katika Shule ya Sekondari Ilenza, ujenzi wa kituo cha polisi, kuchangia madawati na ujenzi wa vyumba vya madarasa," Tinda alifafanua.

Pia alisema shamba limeruhusu wananchi kufanya shughuli za kilimo cha muda mfupi katika maeneo yenye ya uwazi na yenye miche midogo na kutoa ajira kwa wananchi.

Makamu wa Rais wa Shirikisho la Viwanda vya Misitu Tanzania, Fue Kandawala, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye miti iliyosimama pamoja na kupunguza tozo za halmashauri kutoka asilimia tano hadi asilimia tatu.

# Mwinyi ashtuka wizi mabilioni ya fedha

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema anasikitishwa na mambo yanayotokea katika serikali yakiwamo wizi na ubadhirifu wa mali za umma.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu Zanzibar baada ya kupokea ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2020/21 inayoonyesha upotevu wa mabilioni uliofanywa na baadhi ya watendaji wa serikali. Ripoti hiyo iliwasilishwa na CAG Dk. Othman Abbas Ali.

"Nchi haiwezi kwenda namna hii. Kama kuna sehemu kuna wizi tusipochukua hatua, hatuwezi kuwatendea haki wananchi, lazima hatua za msingi zichukuliwe kwa wale wote waliotajwa katika ripoti hiyo," alisema.

Kutokana na madudu hayo, Dk. Mwinyi alitaka Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) kujitathmini upya kuhusu utendaji wake kwa kuwa kiasi kikubwa haijaisaidia serikali katika kudhibiti mianya ya wizi na upotevu wa mapato.

Alisema hajaridhishwa na utendaji wa taasisi hiyo ambayo mwaka jana aliiagiza kuwashughulikia baadhi ya viongozi waliotuhumiwa kujihusisha na wizi wakiwamo wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) waliobainika kuchezea mfumo wa malipo.

"Nasikitika sana nimewaambia ZAECA wafuatilie tuhuma za wizi katika taasisi mbalimbali lakini kwa bahati mbaya sijapata jibu. Wizi unatokea wa waziwazi lakini hakuna anayekamatwa wa au kufikishwa mahakamani," alisema.

Hata hivyo, aliwatoa hofu watendaji wa serikali walioteuliwa wakati akiingia madarakani na kuwataka kuhakikisha matukio na makosa kama hayo hayajitokezi katika ripoti ijayo.

"Nitashangaa sana kama haya yatasemwa mwakani kwani ukiangalia matukio mengi yaliyotajwa hapo ni ya awamu iliyopita ambayo watendaji wetu wameyakuta. Lakini ripoti itakayosomwa mwakani tuhakikishe makosa haya hayajirudii tena," alisema.

Dk. Mwinyi aliipongeza CAG kwa kuweka bayana matukio hayo na kuyataja hadharani kwa ufasaha mkubwa na kusisitiza huo ndio utawala bora.

Alisema serikali itahakikisha ripoti ya CAG inapowasilishwa inasomwa hadharani kwa kuwa huo ndiyo utawala bora wenye lengo la kuweka uwazi wa kila jambo. Alisema kilichoelezwa na CAG ni ukweli na hakina lengo la kumuumbua mtu.

CAG alizitaja kasoro 25 alizozibaini katika taasisi za serikali na mashirika yake hasa katika ununuzi na ukusanyaji wa mapato. Alisema amebaini watendaji wa serikali wakiwamo wahasibu wanachezea mifumo ya fedha, kuisababishia serikali hasara na upotevu wa mabilioni ya fedha.

Akiwasilisha ripoti hiyo, CAG alizitaja wizara zinazoongoza katika upotevu huo kuwa ni ujenzi, mawasiliano na uchukuzi; afya; kilimo, umwagiliaji maliasili na mifugo huku vikosi vya Idara Maalumu SMZ kikiwamo Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM), Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) na Mafunzo vikipata hati chafu.

Aliyataja mashirika ya umma ambayo hati zimebainika kuwa na kasoro nyingi ni pamoja na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA), ZRB, na Mamlaka ya Majisafi na Salama (ZAWA).

Aidha, taarifa hiyo inaonyesha kwamba taasisi saba zina viashiria vinavyoonesha ukiukwaji mkubwa wa matumizi ya fedha kwa mwaka 2020/21, na hivyo kupata hati chafu, taasisi hizo ni KMKM, Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii, Wakala wa Majengo, Kamisheni ya Maafa na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume.

"Taasisi hizi matumizi ya fedha zake hayaridhishi ndiyo maana zimepata hati chafu hatua ambayo inaonyesha baadhi ya wahasibu kuchezea mifumo ya fedha kwa njia za udanganyifu," alisema.

Mdhibiti huyo ameishauri serikali kuhakikisha inakamilisha mchakato wa kutoa maoni ya mapendekezo kuhusu muundo wa tume ya pamoja na fedha ambapo kwa upande wa serikali ya Jamhuri ya Muungano tayari wamekamilisha kazi hiyo.

CAG pia alisema katika ukaguzi wake, amebaini kwamba Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) unahitaji mikakati na mbinu za ziada katika uwekezaji wake vinginevyo uko katika tishio la kupoteza mwelekeo ikiwamo kufilisika.

Alisema katika uwekezaji wa mfuko huo wenye thmani ya Sh. bilioni 10 ikiwamo ujenzi wa mnara na hoteli zilizoko Pemba, hauna tija. Kutokana na hali hiyo, CAG aliitaka Bodi ya ZSSF kujipanga vizuri kuhakikisha miradi inayowekezwa inakuwa na tija.

"Mheshimiwa Rais, tuambizane ukweli ndipo tutapokwenda mbele na kujikwamua na changamoto ziliopo. ZSSF kama haitakuwa makini itakufa kwa sababu haifanyi uwekezaji wenye tija," alisema.

Kuhusu fedha za mfuko wa pensheni, alisema ripoti yake imebainika kuwepo kwa matumizi yasiyofahamika pamoja na utaratibu wa uwekezaji wa fedha kutoka kwa wahasibu ambao ni kinyume cha sheria.

"Kwa mfano Sh. bilioni 75 za wazee za malipo ya pensheni zimepotea baada ya kufanyika malipo hewa. Uchunguzi wetu umebaini kwamba yako malipo hewa yanayofanywa kwa upande wa pensheni jamii wanayolipwa wazee wastaafu pamoja na wastaafu wa kawaida," alisema.

Pia alisema Wizara ya Fedha imeitia hasara serikali kutokana na upotevu wa fedha na ununuzi wa dawa hewa ikiwamo usambazaji wa dawa ambazo katika kipindi kifupi zimemaliza muda wake.

Alisema Wizara ya Fedha kupitia Bohari Kuu ya Dawa, imenunua dawa hewa zenye thmani ya Sh. bilioni tano ambazo katika kipindi kifupi zilibainika kumalizika muda wa matumizi.

Kadhalika, alisema wizara hiyo imelipa Sh. bilioni nne ambazo ni deni danganyifu kwa wazabuni waliokuwa wakisambaza dawa kwa Wizara ya Afya.



Naibu Spika wa Bunge, Mussa Azzan 'Zungu' (kulia), akisalimiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, Ludovick Utouh, kabla ya kufungua mafunzo ya uwazi na uwajibikaji kwa Kamati za Usimamizi za Bunge za PAC, LAAC na PIC, pamoja na Kamati ya Bajeti, jijini Dodoma jana. **PICHA: BUNGE**

# Mapingamizi kesi ya Anglikana yatupwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TUME ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) imetupilia mbali mapingamizi yaliyowasilishwa na Baraza la Wadhamini wa Kanisa la Anglikana Tanzania dhidi ya kesi ya msingi iliyofunguliwa na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Kanisa hilo aliyefukuzwa kazi Juni mwaka huu, Dk. Mecka Ogunde.

Kutokana na kutupwa kwa mapingamizi hayo CMA imeamua kesi ya msingi iliyofungulia na katibu huyo ianze kusikilizwa Septemba 13, mwaka huu.

Dk. Ogende alifungua kesi ya msingi CMA kulishtaki baraza hilo baada ya kumfukuza kazi bila kufuata sheria na kumnyima stahiki zake zote.

Julai 27, mwaka huu, akizungumza na waandishi wa habari Wakili wa Mlalamikaji, Willison Ogunde, alisema shauri walilofungua ni CMA/DOM/84/2022 ambapo mteja wake ambaye alikuwa Katibu Mkuu wa Kanisa Aglikana Tanzania analalamikia ajira yake kusitishwa bila kufuatwa sheria na bila sababu ya msingi na kukosa haki zake zote.

Baada ya kiongozi huyo kufungua shauri hilo, upande wa mlalamikiwa uliwasilisha hati kinzani.

Ambapo Agosti 10, mwaka huu, pande zote zilitoa maelezo yao mbele ya Msuluhishi Mwandamizi (CMA) Mkoa wa Dodoma, Rodney Matalis, ambaye alisema uamuzi wake ungetolewa Agosti 26, mwaka huu kama mapingamizi hayo yangekubaliwa au kutupiliwa mbali.

Mapema juzi, Msuluhishi Mwandamizi Matalis alitoa uamuzi wa kuyatupilia mbali mapingamizi ya Baraza la Maaskofu Kanisa la Anglikana Tanzania kutokana na kutokidhi matakwa ya kisheria.

Baada ya uamuzi huo mlalamikaji Dk. Ogunde, alizungumza na waandishi wa habari, akisema huo ni mwazo mzuri kwake kupata haki ambayo kanisa hilo lilimpoka.

Wakili wa walalamikiwa, Sostenes Mselengwa, alisema mapingamizi yao yaliyotupiliwa mbali yalilenga kupinga CMA kushughulikiwa suala hilo kwa madai kwamba haina mamlaka ya kusikiliza shauri hilo kwamba ilifaa litatuliwe na Kanisa Anglikana Tanzania.

Alidai kuwa mlalamikaji alipaswa baada ya kuondolewa na nyumba ya maaskofu, kwenda kwenye Baraza la Rufani.

Mgororo huo wa kanisa ulianza mara baada ya Baraza la Wadhamini wa Kanisa hilo kumwondoa madarakani kiongozi huyo kwa madai ya kuwa nje ya ofisi kwa muda mrefu mapema mwezi Juni mwaka huu.

Dk. Ogunde alilazimika kufungua kesi kulishtaki Baraza la Wadhamini huko CMA baada ya kushindwa kufikia makubaliano na uongozi wa kanisa kuhusu stahiki zake.

# Mchimbaji anasa tanzanite ya bil. 2/-

**Na Jaliwason Jasson,** SIMANJIRO

MCHIMBAJI wa madini ya tanzanite katika Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Anselim Kawishe, ametangazwa kuwa bilionea mpya wa madini ya tanzanite.

Kawishe amekuwa bilionea mpya baada ya kupata vipande viwili vya madini hayo vyenye thamani ya Sh. bil. 2.2/-

Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Adolf Nduguru, alimtangaza bilionea huyo jana Mji Mdogo wa Mirerani katika hafla ya ununuzi wa madini hayo.

Alisema Kawishe alipata vipande viwili vya madini ya tanzanite vyenye uzito wa kilogramu 3.74 na kilogramu 1.48, mtawalia.

"Kati ya madini hayo, yenye uzito wa kilogramu 1.48 yana thamani ya Sh. milioni 713.8 na ya uzito wa kilogramu 3.74 yana thamani ya Sh. bilioni 1.5, hivyo kufanya jumla ya Sh. bilioni 2.245," alisema Nduguru.

Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, alimpongeza Kawishe kwa kufanikiwa kupata madini hayo.

"Hata mimi nisipokuwa bilionea, wananchi wangu wakiwa mabilionea ndiyo na mimi ninafarijika, tumezidi kuzalisha mabilionea wapya," alisema Ole Sendeka.

Mchimbaji wa Madini ya Tanzanite, Sokota Mbuya, alisema serikali inapoweka sheria rafiki za uchimbaji, ndipo inaposaidia kuzalisha mabilionea wapya.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kodi ya zuio iungwe mkono ili kuharakisha maendeleo

**KATIKA** siku za karibuni umeibuka mjadala mzito juu ya tozo zinazotokana na kodi ya pango baada ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kutoa taarifa kuwa itaanza kufuatilia ulipaji wa kodi hiyo, maarufu kodi ya zuio.

Kimsingi, kodi hiyo ni asilimia 10 ya fedha anazolipa mtu kwa ajili ya pango ama kwa ajili ya biashara au makazi. Awali, kodi wanatozwa wale waliokuwa wakipokea au kulipa Sh. 500,000 na kuendelea lakini sasa watu wote wanaopangisha sehemu zao, watatakiwa kulipa pasi na kujali kiwango kinachotozwa.

Hatua hiyo imeibua mjadala kutoka kwa watu hata kuanza kuitupia lawama serikali kuwa inawaonea na kuwanyanyasa wananchi kutokana na mlolongo wa tozo katika maeneo mbalimbali.

Baadhi ya watu waliotoa maoni kuhusu kodi hiyo, wamesema tozo zinazidi kuongezeka wakitolea mfano kwenye miamala ya simu, benki na katika bidhaa mbalimbali. Watu hao wamekwenda mbali zaidi kwa kusema serikali haijali watu wake kwa kuibua tozo mbalimbali ambazo zinakuwa mzigo kwao.

Pamoja na malalamiko hayo kuhusu kodi hiyo, ni ukweli usiopingika kwamba tozi hiyo imekuwapo kwa muda mrefu bali serikali ilichofanya kupitia TRA ni kuwakumbusha wananchi umuhimu wa kuilipa na kwamba iko kisheria na kikanuni kama zilivyo kodi zingine. Ziko taasisi ambazo zimekuwa zilikipa miaka nenda rudi kutokana na upangishaji wa majengo ya makazi au biashara. Miongoni mwa taasisi hizo ni Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Shirika la Nyumba la Taifa ambazo zimekuwa zikipangisha majengo yao ama kwa makazi au kwa biashara.

Hata baadhi ya wafanyabiashara na wajasiriamali wanaopanga katika maduka au vyumba vya watu binafsi jambo hilo si geni kwao kwa kuwa kila wanapoenda kukadiriwa kodi TRA, wanatakiwa kuonyesha mikataba ya pango na hatimaye kulipa asilimia 10 ya kodi ya pango waliyolipa. Kwa mantiki hiyo, kodi hii ipo kwa muda mrefu lakini ufuatiliaji umekuwa mdogo, hivyo kusababisha serikali kukosa mapato au kukusanya kiasi kidogo kutokana na aina hiyo ya kodi.

Serikali kupitia TRA inastahili pongezi kwa kuhimiza ulipaji wa kodi hiyo na jambo hilo lisiishie hapo tu bali litekelezwe kwa vitendo. TRA, kwa kuanzia maeneo ya mijini ambako kuna biashara ya upanghishaji majengo, inapaswa kuanza ufuatiliaji wa karibu mtaa kwa mtaa ili kuhakikisha kodi hiyo ya zuio inalipwa ipasavyo.


Iko mifano mingi ya baadhi ya maeneo ambayo kodi hiyo hailipwi licha ya kwamba wamiliki wa nyumba wanachukua mamilioni ya fedha huku serikali ikikosa mapato. Katika eneo la Mikocheni, kwa mfano, kuna mtu anamiliki nyumba yenye sehemu tatu za kupangisha (apartment) na kwa mwezi anatoza Dola za Kimarekani 1,500 kwa kila sehemu. Swali la kujiuliza ni je, analipa kodi stahiki ya zuio kutokana na upangishaji huo?

Huo ni mfano mmoja tu lakini kuna watu wengi wanaopangisha nyumba na hawalipi kodi ya zuio, hivyo Watanzania tunapaswa kujiuliza serikali inakosa fedha kiasi gani ambazo kama zingekusanywa kikamilifu au hata kwa asilimia 50 tu, miradi mingapo ya maendeleo ingetekelezwa bila kutegemea misaada na mikopo kutoka nje?

Kama kweli tuna uzalendo wa kweli kwa nchi yetu, ni vyema tukaiunga mkono serikali kwa kusisitiza kodi hii ya zuio ikalipwa na kukawa na usimamizi thabiti ili kupata fedha kwa ajili ya masuala ya maendeleo. Lengo la serikali kuhimiza kodi hii ni zuri kwa sababu fedha zitakazopatikana zitaelekezwa katika ujenzi wa shule, vituo vya afya na zahanati, barabara na miradi ya kimkakati na hatimaye taifa kuwa na maendeleo ya kiwango kizuri kiuchumi na kijamii.

Ili kuhakikisha azma ya ulipaji kodi hiyo inatimizwa kikamilifu, ni muhimu ikaanzishwa kampeni kabambe ya utoaji elimu kwa umma pamoja na kuweka bayana adhabu ambayo mtu anaweza kuipata kutokana na kukwepa au kukaidi kulipa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

# Kesho zamu yenu mliokiuka marufuku mifuko ya plastiki

Na Sabato Kasika

**OPERESHENI** ya kusaka wale wanaouza mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku inatarajiwa kuanza kesho mkoa wa Dar es Salaam, kwa ajili ya kutekeleza maekelezo ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Makamu wa Rais ameelekeza kufanyika msako mikoa yote, ili kuwanasa wale wote wanaoiingiza kutoka nje ya nchi na wenye viwanda bubu vinavyotengeneza mifuko hiyo iliyopigwa marufuku tangu Juni Mosi. 2019.

Katika utekelekezaji wa maelekezo ya Makamu wa Rais, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam , Amos Makalla, ametangaza kuwa Agosti 29, yaani kesho ni siku rasmi ya kuanza operesheni hiyo.

Ikumbukwe kuwa tangu mifuko hiyo ipigwe marufuku, vilianza kuzalishwa vifungashio mbadala, ambavyo vinapatikana kwa wingi maeneo mbalimbali kuanzia kwenye masoko hadi madukani.

Lakini cha kushangaza ni kurejeshwa kwa mifuko hiyo inayoingizwa kutoka nje ya nchi, huku ikielezwa kuwa mingine inatengenezwa nchini na viwanda bubu vinavyomilikiwa na baadhi ya wafanyabiashara.

Ninadhani haikuwa na haja ya kulazimisha kuwapo mifuko ambayo imepigwa marufuku, kwani kitendo cha kuiingiza nchini kinyemela au kuizalisha katika viwanda bubu ni sawa na kutaka kutii sheria kwa shuruti.

Hatua iliyochukuliwa na serikali Juni mosi mwaka 2019, ingetosha kuzingatiwa, kwani tayari mifuko mbadala ya kubebea vitu inazalishwa kwa wingi, hivyo wangeheshimu uamuzi huo wa serikali.

Mtindo wa baadhi ya watu kutaka kutii sheria kwa shuruti, inafanya serikali ya mkoa wa Dar es Salaam kuelekeza maelekezo ya Makamu wa Rais kwa ajili ya kunusuru afya za watu na mazingira.

Huwa inaelezwa kuwa mifuko hiyo ina madhara kiafya, lakini inaharibu na kuchafua mazingira, hivyo ingekuwa ni vyema iwapo hao ambao wamekiuka marufuku ya serikali wangejali hayo.

Kutotii kwa baadhi ya wafanyabiashara, kunaifanya serikali ya mkoa wa Dar es Salaam kuelekeza kila wilaya kupitia kamati za ulinzi na usalama kuendesha operesheni hiyo, huku maofisa masoko wa wakitakiwa kutoa taarifa kila siku ya mwenendo wa operesheni hiyo kwa mkurugenzi wa halmashauri husika.

Mamlaka za udhibiti likiwamo Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), zimeagizwa kutoa tamko la maelekezo ya usimamizi kwa kila mkoa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha elimu inaendelea kutolewa kuhusu athari za mifuko iliyopigwa marufuku.

Ingekuwa vyema kama wahusika wakachukua hatua mapema za kuachana na biashara iliyopigwa marufuku, ili kuepuka kubanwa na vyombo vya dola, kwani matokeo ya kutotii sheria ni kulazimishwa kutii.

Hatua hiyo inaweza kutafsiriwa kuwa wanaofanya hivyo wameamua kuibipu serikali, ambayo na sasa na yenyewe imeamua kuwapigia, hivyo ni wazi kuwa kesho wanaweza kukutana na shuruti.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ameshatangaza kuanza msako wa mifuko hiyo kesho huku akiwataka viongozi wa masoko yote kutoa tangazo la katazo la uuzaji wa mifuko hiyo kabla ya operesheni.

Kwa mujibu wa Makalla, viongozi wa masoko, machinga na maofisa masoko wanatarajiwa kushiriki katika operesheni hiyo, ili kusaidia kunasa wahusika ambao wameamua kukiuka maelekezo ya serikali.

Binafsi ninaamini kuwa hatua ya serikali kuanzisha operesheni, ingetosha kuwakumbusha wale walioanza kurejesha mifuko hiyo kutambua kuwa imedhamiria kuifuta nchini, hivyo asiwapo anayeiuza au kuinunua na kuitumia.

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Hongera mliohesabiwa, ambao bado tutahesabiwa kweli?



Na Pascal Mayalla

LEO ni siku ya sita ya Sensa ya Watu na Makazi kwa ajili ya nchi kupata idadi kamili ya watu wake ili kuwa na uwezo wa kupanga mipango ya maendeleo kwa umakini kupitia takwimu zitakazopatikana.

Jambo hilo limekwenda vizuri kulingana na taarifa licha ya kwamba baadhi yetu hatujafikiwa mpaka sasa ili tupate kuhesabiwa. Hatua hiyo inanifanya kujiuliza swali je, ambao hatujahesabiwa, tutahesabiwa kweli?

Ninasema hivyo kwa sababu hamasa ilikuwa kubwa sana kiasi kwamba tukajiandaa vilivyo kwa ajili ya tukio hilo adhimu. Ukihamasisha jambo na watu wakajitokeza, siku ikirudi anza na kuwapongeza waliojitokeza ndipo uulize sisi ambao bado, tutahesabiwa kweli?

Ama kweli, mkamia maji, hayanywi! Waswahili walisema, jambo ukilipania sana haliwi! Inawezekana hii sensa mimi niliipania sana! Kwa wiki tatu mfululizo kabla ya sensa, safu yangu hii ilijikita kwenye kuhamasisha sensa. Sasa sensa yenyewe imefika, mimi sikuhesabiwa! Leo ni siku ya sita bado sijahesabiwa!

Nimeshiriki sensa nne ya mwaka 1978, 1988, 2002 na ya mwaka 2012. Sensa ya mwaka huu ndiyo ya kwanza kutohesabiwa ile siku ya sensa yenyewe na mpaka jana wakati naandika makala hii ilikuwa siku ya tano tangu kuanza kwa mchakato huo na kaya yangu pamoja na mtaa wangu bado hatujafikiwa.

Siku ya sensa niliianza vizuri kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania. Rais Samia Suluhu Hassan, au Mama kama tulivyozoea kumwita, alinitumia ujumbe mfupi wa maandishi, kuhusu Sensa. Uliosomeka hivi: "Mimi Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nakukaribisha kushiriki sensa tarehe 23 Agosti, 2022. Nakusihi utoe taarifa sahihi."

Mimi niliupata ujumbe huu, wewe mwenzagu, pia uliupata? Ulijisikiaje kupokea ujumbe mfupi wa maandishi kutoka kwa Rais wa nchi kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu? Nani mwenye kumbukumbu yoyote ya Rais wa JMT kuwahi kutuma ujumbe wowote kuhusu jambo lolote?

Si lengo la makala hii kuingilia kazi ya makarani wa sensa lakini kwa vile sensa zote zilizopita, ulikuwa unahesabiwa siku ya kwanza, hivyo ile siku ya kwanza unakuwa umeipania sana. Kila ukisikia mlango kugongwa, siku zote ni kumtuma dada kufugua geti, lakini siku hiyo ni baba mwenyewe unakwenda kufungua ili uwapokee mwenyewe makarani. Kusikia tu geti linagongwa, baba mbio kwenda kufungua na kuwakaribisha makarani wa sensa.

Kufika getini na kufungua geti la haula! Kumbe ni mama wa mboga! Nusu ubamize mlango na kutaka kumfurusha mama wa watu kuwa leo hatununui mboga. Mama wa mboga anamuulizia dada kama leo tunachukua, kumbe dada kamsikia na kuja getini. Anamjibu tunachukua, pesa utapitia baadaye!

Mama wa mboga naye anasema leo nimepita mapema zaidi ili nimalize mapema na mimi niende kwangu kusubiri kuhesabiwa, hivyo naomba pesa kabisa maana leo nikipita nimepita sirudi tena njia hii. Uzuri wa waleta bidhaa wa nyumbani siku huna wataacha na kesho yake watapitia. Hivyo dada akamwambia tunachukua utapitia kesho! Siku hiyo ndiyo baba unashuhudia mboga zikinunuliwa, kisa ni kuwasubiri makarani wa sensa.

Kwa vile sensa zote za nyuma, umezoea kuhesabiwa siku ya kwanza, sijui kama ilikuwa bahati tu lakini kaya zingine zilikuwa zinahesabiwa kwa siku saba sijui! Lakini sensa hii leo siku ya sita nina haki ya kujiuliza kama leo au kesho nitafikiwa kweli.

Nikilinganisha zile sensa zingine na hii ya leo, kiukweli kabisa na kwa dhati ya moyo wangu, kuna tatizo mahali. Hakuna mtu anaujua mtaa wake kuliko mjumbe wake wa nyumba 10. Hakuna mtu anaujua mtaa wake kuliko serikali yake ya mtaa, nyumba yangu ni hatua chache kutoka ofisi ya serikali ya mtaa wangu. Haiwezekani leo ni siku sita makarani wa sensa hawanifikii, wakati inawachukua nusu siku tu kwa watu wa serikali ya mtaa wangu kuwafikia wakazi wote wa mtaa wangu. Kwa nini hawa makarani wa sensa hawakuwa wajumbe wetu wa nyumba 10 na maofisa wetu wa serikali za mtaa?

Kama Tanzania sasa tuna vitambulisho vya taifa, vyenye 'biometric data' na tuna serikali mtandao, nini faida ya vitu hivyo? Nimemsikia Kamisaa wa Sensa Mama Anne Makinda, akisema tungekuwa nchi za wenzetu, tungejihesabu na kutuma data. Mbona kuna sisi Watanzania wengi tu tuna simu janja, tuna vitambulisho vya taifa, nchi yetu ina serikali mtandao, si wenye uwezo wa kujihesabu na kutuma data tungetuma na karani angepita tu kuhakiki kwa dakika chache? Zile sensa za kuhesabiwa kianalojia tumehesabiwa kwa siku moja, leo tunahesabiana kidigitali, tunasubiri siku sita tuhesabiwe, hapa hakuna tatizo?

Mbona kwenye E Passport tumeweza, E Visa tunaweza, E registrations tumeweza, TRA tunafanya E-Filing, tunashindwa vipi kwenye kitu kidogo kama kujihesabu tu?.

Pamoja na matatizo yote, kwenye mazuri pia tupongeze, naipongeza Televisheni ya Taifa kutulea matangazo mubashara ya sensa, tukashuhudia ile siku ya kwanza ya sensa ya viongozi wakihesabiwa na mpaka leo wananchi tukihesabiwa. Hongera sana Dk. Ayoub Rioba na timu yako kwa kazi nzuri.

La mwisho, mfumo wa kidigitali unarahisisha sana kazi. Tukijenga mifumo imara, hatuhitaji hii 'duplicity' ya vizazi na vifo, RITA, vitambulisho vya taifa, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Uhamiaji, vunja haya mavitu yote, weka vitu vyote katika mfumo mmoja. Hata ukusanyaji wa kodi, hakuna tena kushikana mashati. Kila kitu kimewekwa katika mfumo wa pamoja.

**Nasubiria Kuhesabiwa!**

**Wasalaam**
**+255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tutaanza kutafuta elimu ya kuhifadhi fedha benki!



Na Joseph Kulangwa

BILA shaka Watanzania wenzangu mnamaliziamalizia Sensa ya Watu na Makazi yenye mafanikio na kama haimaliziki maliziki, basi wahusika wenye mamlaka wataamua lifuatalo, ili kufikia pazuri.

Pamoja na ya hapa na pale katika kukamilisha sensa, hasa yale ya kusikia vishikwambi vimeibwa au kupotea, yale ya kusikia karani kahesabu kaya moja na kuishia kwenye viti virefu na kutoka tilalila, bado tumefanikisha jambo letu.

Penye kundi la watu hapakosekani kasoro za hapa na pale, kwa sababu binadamu tunatofautiana kizazi kimoja hadi kingine, rika moja na lingine na hata tabia moja na nyingine.

Wako waliodhani sensa ni mahali pa kupata kivuno, ndio hao waliopigiana pande mtoto wa fulani apate au kijana wa chama fulani mshika kishikwambi bila hata kuzingatia vigezo au sifa, na matokeo yake ni kulizwa vishikwambi.

Watu hawajui kuwa vishikwambi hivyo bado vitatumika baada ya sensa kwa kupewa kundi fulani la wataalamu wetu wa kutuelimisha, ili fedha zilizotumika kuvinunua zisiishie kwenye sensa, hivyo waliovipoteza makusudi wametukosea sana. Bila shaka dola itajua la kufanya.

Ila pengine niseme kama tulivyokuwa tukifanya zamani, tukiamini walimu wetu hata katika kutusimamia uchaguzi, naamini bado wengi wa walimu ni waaminifu na waoga kama si wacha Mungu, kuliko kuokoteza watu kufanya kazi nyeti kama hizi.

Zamani mwalimu alitambulika tu kwa wajihi na mwenendo wake kama si mwonekano. Enzi za mwalimu kuvaa kaptula na soksi ndefu tukiziita stokingi zilizochomekwa kalamu ya Bic, wei kichwani, kama aliongeza miwani basi alikuwa bonge la ticha.

Enzi hizo kazi ni ualimu ndiyo iliyokuwa ya heshima katika jamii kabla haujadharauliwa na kuonekana kama ndiyo kazi ya aliyekosa kazi. Hapo ndipo tulipoanza pia kuwatenga katika kazi kama hizo za uchaguzi na sensa, bila shaka wangefanya vizuri kabisa, kwa kushirikiana na viongozi wa serikali za mitaa. Tuyaache hayo yamepita.

Sambamba na hilo, nakumbuka zamani tukihimizwa kuweka au kuhifadhi fedha zetu benki, ingawa hazikuwa nyingi lakini zilikuwa na thamani, hivyo tukiambiwa kuzihifadhi na kutumia kidogo kidogo, kwani haba na haba enzi hizo ilijaza kibaba.

Nakumbuka wakati huo tukiweka fedha benki tulikuwa tukiongezwa kitu faida, hivyo tukikimbilia benki tukichelea kulala na fedha uchagoni, kwamba inaweza kutokea siku moja panya wakafanya yao ukaingia hasara, au moto ukafanya yake ukalizwa au hata mvua ikanyesha fedha zikaloa.

Ni enzi ambazo haikuwa rahisi kumtumia mtu fedha mpaka aagizwe kondakta wa basi au dereva kama si kumtuma mtu ukamlipia nauli akapanda basi kupeleka fedha kijijini, kama si kukodi baiskeli kupeleka kwa wazee.

Ndio wakati huo pia tukiandika barua sana ili kujuliana hali na kuipeleka kwenye mabasi kama si Posta, maeneo kulikokuwa na ofisi za posta. Simu nazo zilikuwa za kufuatilia Posta ili kuhudumiwa na ukibahatika labda ofisini kwa mtu, kulikokuwa na simu za kukoroga.

Hata ukitaka kuonana na mtu enzi hizo unamfanyia unamjulisha mapema kuwa kesho saa fulani tuonane na kama mmoja akichelewa ilikuwa kasheshe na wakati mwingine asifike na huwezi kumuuliza umepatwa na nini. Ila uaminifu ulikuwa mkubwa na kila miadi ilitimia.

Pole pole sasa teknolojia ikaja, simu zikahamia mkononi na mawasiliano yakawa rahisi, unaongea na mtu aliye mbali nawe kama yuko hapa. Matumizi ya barua yakapungua. Tukatuma fedha kwa simu bila wasiwasi.

Tukaendelea kuweka fedha benki, lakini sasa huko benki mambo yakabadilika, kama zamani tukiweka fedha na baada ya muda tukipata angalau kijifaida, leo tunakatwa kama malipo ya huduma ya kutunziwa au kuhifadhiwa fedha yako benki.

Kwa hiyo tofauti na zamani ambako ukiweka 10 ulitoa 15, leo ukiweka 15 unatoa 10. Makato kila mahali, tozo benki tozo kwenye miamala ya simu. Watu tunagugumia pengine bila kujua nini maana yake, lakini bila shaka kuna maana yake. Tunahitaji tu elimu.

Nadhani tusitazamane kwa macho mekundu na kutafutana uchawi miongoni mwetu. Bado tuna muda wa kupeana elimu ya nini kifanyike katika hili ili watu wasijeona kuwa pengine benki hazina faida na kuanza tena kulalia fedha uchagoni na kujiingiza katika hatari ya kupata hasara. Wenye dhamana bila shaka mpo, fanyeni kazi yenu mumsaidie Chifu Hangaya. **Alamsiki!**

# Mbaroni tuhuma za mauaji

**Na Samson Chacha,** TARIME

JESHI la Polisi Mkoa wa Tarime Rorya linawashikilia wakazi wawili wa Kitongoji cha Buhemba, Kijiji cha Ngereng'ere, Kata ya Regicheri kwa tuhuma za mauaji ya Matinde Masaite, aliyekatwa panga shingoni.

Watuhumiwa hao ni James Bhoke Siang'awi na Mwita Kerongwe.

Kamanda wa Polisi Mkoa huo, Geofrey Sarakikya, alisema jana kuwa walifanya uchunguzi kwa kushirikiana wa wananchi na kuwakamata watuhumiwa hao.

"Masaite aliuawa wiki iliyopita kwa kukatwa panga shingoni na mwili wake ukitupwa jirani na nyumbani kwake.

Tunaendelea na uchunguzi zaidi kuhusiana na tukio hili na upelelezi ukikamilika tutawafikisha katika vyombo vya sheria ili kujibu tuhuma zinazowakabili za mauaji," alisema.

Kamanda Sarakikya alitoa onyo kwa wananchi wanaojichukulia sheria mikononi kwa kufanya vitendo vya uhalifu.



Mwakilishi Mkaazi wa IMA-World Health Tanzania, Lali Chania, akichangia mada katika mkutano wa 10 wa kutengeneza mpango kazi wa mwaka 2022/23 wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mahakama yapunguza mrundikano mashauri

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MAHAKAMA imesema imefanikiwa kupunguza mrundikano wa mashauri mahakamani huku idadi ya matukio makubwa ya uhalifu wa kusisimua ikipungua.

Hatua hiyo inakuja baada ya mahakama hiyo kuunda kikosi kazi cha mahakimu sita kuangalia namna ya kupunguza mrundikano wa mashauri.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Shinyanga, Athumani Matuma, aliyasema hayo juzi kwenye hafla ya kutunuku vyeti vya pongezi kwa kikosi kazi cha mahakimu hao kutokana na kazi kubwa waliyoifanya ya kupunguza mrundikano wa mashauri mahakamani kwa muda mfupi.

Mahakimu waliotunukiwa vyeti ni Mohamed Richard, Christiani Rugumila, Christina Chovenye, Catherine Langwa, Enos Misana na Sayi Mabondo.

Wengine waliotunukiwa vyeti vya pongezi ni Ofisa Tawala Mahakama ya Wilaya ya Kahama, Boniface Fumbe, Dotto Mabula, Ofisa Tawala wa Mahakama ya Kishapu na Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Simiyu, Chema Maswi.

Jaji Mfawidhi Matuma alisema mahakama hiyo ilibuni mbinu hiyo huku mahakimu hao wakifanya kazi hiyo kwa kujitolea kwa kutembelea kila mahakama.

"Kikosi kazi hiki tulikiunda mwezi Februari mwaka huu, lakini ndani ya muda mfupi kimeleta matunda na kupunguza mrundikano wa mashauri mahakamani na tunawatunuku vyeti kutokana na kazi kubwa ambayo wameifanya.

"Kazi ya kutembelea katika Mahakama za Wilaya na Mkoa kushughulikia mrundikano wa mashauri imesaidia sana, sisi hapa Mahakama Kuu Kanda ya Shinyanga tulikuwa na kikosi chetu na kati ya mashauri 56, tumeshughulikia 46 na sasa yamebaki mashauri 10," alisema.

Pia alisema wamejipanga kuyashughulikia mashauri 62 ili ifikapo Desemba mwaka huu, yawe yamebaki machache.

Kiongozi wa kikosi kazi cha mahakimu hao, Mohamed Richard, alisema walianza kushughulikia mrundikano wa mashauri katika Mahakama ya Wilaya ya Bariadi kwa kusikiliza kesi 43 na Mahakama ya Wilaya ya Maswa kesi 11.

Alisema kazi hiyo itakuwa endelevu ili kupunguza mrundikano wa mashauri na kuwatendea haki wananchi kwa muda mfupi.

Alisema katika Mahakama Kuu shauri linatakiwa kushughulikiwa ndani ya miaka miwili, ngazi ya mkoa mwaka mmoja na wilaya miezi sita.

Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Ramadhani Kingai, alisema katika kuimarisha haki, vipaumbele vya serikali ni kupunguza uhalifu na mrundikano wa mashauri mahakamani yakiwamo ya jinai.

Kingai alisema kwa sasa nchi ni salama na hakuna matukio makubwa ya uhalifu.

Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Antony Mwakitalu, alipongeza Mahakama Kuu Kanda ya Shinyanga kwa ubunifu huo na kubainisha kuwa bila haki, hakuna amani wala maendeleo.

Alisema ofisi yake itapeleka mahakamani mashtaka yaliyokamilika ili mashauri yamalizike kwa wakati.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, alisema kupunguza mrundikano wa mashauri mahakamani ndiyo kiu ya Watanzania na kukipongeza kikosi hicho kwa kutanguliza uzalendo.

# Uwekezaji waja makazi ya wazee

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

SERIKALI kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, imejipanga kushirikiana na wizara za kisekta na wadau mbalimbali kuboresha huduma katika makazi ya wazee nchini.

Mpango huo ni pamoja na kutathmini matumizi ya ardhi na kuona fursa zilizoko kwa ajili ya kuanzisha miradi ya kimkakati kwenye maeneo hayo.

Hayo yalibainika juzi wakati wa ziara ya manaibu makatibu wakuu kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara katika makazi ya wazee ya Fungafunga mkoani hapo.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Amon Mpanju, alisema serikali imekuja na mikakati ya kuwekeza miradi mbalimbali ya maendeleo na kuwataka wananchi wanaozunguka maeneo hayo kutovamia ili yabaki kwa ajili ya kuhudumia wazee.

Mpanju aliwasihi wazee kujitokeza katika Sensa ya Watu na Makazi inayoendelea ili kuwa na takwimu sahihi zitakazosaidia serikali kuweka mipango na mikakati kwa ajili ya kuwahudumia.

Naye Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI (Afya), Dk. Grace Magembe, amesema wazee ni hazina na serikali itaendelea kuwatunza na kuwahudumia ili kuhakikisha wanaishi katika amani na utulivu kwa kuwawekea mazingira salama.

Alisema suala la kuwatunza wazee ni la jamii, hivyo jamii iwajibike kuwalea na kuwatunza na kuona jukumu hilo ni la jamii nzima kwa kushirikiana na wadau.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Hashir Abdalah, alisema kwa upande wake, wizara hiyo itashirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii ili kuhakikisha maeneo ya makazi hayo yanatumika katika kuanzisha miradi ya kimkakati.

Ameongeza kuwa maeneo yaliyoko katika makazi hayo yanaweza kutumika kwa ajili ya kuwekeza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa maslahi mapana ya kuwahudumia wazee katika makazi hayo kutokana na mapato ya miradi hiyo.

Akitoa taarifa ya makazi ya Wazee FungaFunga, Ofisa Mfawidhi wa makazi hayo, Rehema Kombe, alisema makazi hayo yanahudumia wazee 21 kwa sasa ambao wanapatiwa huduma muhimu za malazi, chakula, huduma za afya na msaada wa kisaikolojia kwa wazee hao.

Aliongeza kuwa makazi hayo mbali na kuwahudumia wazee, lengo ni kuwa na mradi wa kulima mboga kwa kuhusisha makazi hayo na wananchi wanazunguka eneo hilo.

# MAISHA

AGOSTI 28, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 15

## Usifanye makosa unapojenga nyumba ili kuepuka kuvuja



Ukurasa 14

## MIHOGO NA CHACHANDU




## KATUNIKA


Ukurasa 16




# LAZIMA WAKUGANDE

Ukurasa 13


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | J | U | M | B | A |
| | A | | | O | |
| U | M | O | | M | |
| | B | | P | A | A |
| | I | | | N | |
| K | A | M | B | I | |


## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
IBA, ONA, YANGA, DIMBA, BAMBIA, DONYOA

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

MTOTO John alikuwa na bibi yake sebuleni wakiongea, ghafla panya alipita karibu yao na kukimbilia nje ya nyumba.

John alijaribu kumkimbiza ili amuue lakini alishindwa kutokana na panya kuwa na kasi kubwa. Alipoona ameshindwa alirudi kwa bibi yake na alimuuliza.

John: Bibi eti panya nasikia anakula watu na kupuliza?

Bibi: Hapana mjukuu wangu, panya hali watu

John: Mbona mwalimu alisema panya anauma na kupuliza?

Bibi: Mwalimu hakuwa na maana hiyo, alimaanisha kwamba mtu kufanyiwa jambo huku hatambui kama baya kama anavyofanya panya anapong'ata usiku bila mtu kutambua.

SWALI
Mamba makazi yake yapo wapi?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Waganga wa jadi walivyoua mwelekeo wa maisha yangu - 3

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na kisa cha kijana Selestine alivyojikuta kwenye anga za waganga wa jadi akisaka utajiri. Hii ni sehemu ya tatu ya simulizi yake kwa yale aliyopitia ambapo alijikuta kwenye pango la nyoka mkubwa alikopelekwa na mganga.

Makala mbili zilizopita, alielezea masharti kadhaa ya mganga likiwamo kumletea kamba ya mtu aliyekufa kwa kujinyonga. Sharti hili ilibidi asafiri kutoka Rwanda kuja Tanzania kuisaka kamba hiyo na kuipata.

Mganga akaikataka na kutia vipande hivyo kwenye kikaango chenye makaa ya moto, akatia na udi. Kisha akampa karatasi nyeupe na kalamu nyekundu aandike majina yake matatu. Halafu aandike maneno yafuatayo;- "nakuandikia wewe mfalme mkuu wa uweza wa anga mwenye utajiri wote na fahari zote, naomba unipe utajiri".

Anaendelea kueleza kijana huyu kuwa, mganga aliniambia nikae hapo Rwanda kwani kuna watu watakuja usiku lakini usiogope. Kweli siku ya tatu upepo ukavuma sana nikaona nyumba yote imejaa upepo.

Baadaye nikaona taa au balbu ya kile chumba imebadilika. Mwanzo mwanga ulikuwa mweupe na kuwa wa bluu, mwili ukaanza kusisimka. Ndipo wakatokea watu wawili pembeni wananisemesha ambao walikuwa ni mganga na mtu mwingine.

Selestine anaendelea kueleza kuwa yule mganga akamwambia wewe kweli ni mwanaume. Kisha akampa mafuta lita tano ambayo naweza kujipaka na kwenda sehemu yoyote bila kuonekana.

Na mafuta hayo pia yanatumiwa sana na watu mbalimbali wakiwamo viongozi mashuhuri. Nayo hupatikana chini ya bahari, Ziwa Tanganyika na hata Ziwa Victoria.

Akaniambia nitakuwa najipaka mafuta hayo kwa kuchanganya na unga wa sembe usiku na asubuhi. Na wakati huo niwe naangalia mashariki na nitakuwa nafanya hivyo kwa mwezi mmoja. Pia mafuta yasikae ndani kwani nitakuwa na vita na wachawi kwa kuwa nitakuwa nawaona.

Baada ya mwezi mmoja ukiwa unamsalimia mtu mpe mkono wa kushoto na kama unampa kitu mpe pia kwa mkono wa kushoto au umwekee juu ya meza.

Baada ya mwezi unapotaka kusafiri, mfano safari ni kesho, nunua bakuli la chuma au sufuria mpya isiyopungua ujazo wa lita moja weka maji kuanzia saa 9:00 alasiri hadi 12:00 jioni.

Hapo ukiwa na kapeti jekundu kama unafanya ibada kwa muda wa dakika tano. Paji la uso na kidevu viguse kwenye maji. Kisha useme maneno yafuatayo;- Enyi wazee mliolala mahali pema mnisikilize mjukuu niingiapo na nitokapo mnifikishe katika safari yangu ninakoenda. Baada ya maneno hayo utakunywa maji kidogo na kutema Magharibi, Mashariki na Kaskazini.

Baada ya kunipa hayo mafuta kabla sijarejea Tanzania, mganga akaniambia wewe nyota yako inaonekana ni kubwa mno. Sasa kuna sehemu nitakupeleka kwa mzee. Kwa mawazo yangu nilifikiri ni kwa mganga mkubwa wake.

Tulipokwenda ni pori yaani msitu mzito, una mlima mkubwa wenye pango. Tulipokaribia lile pango, mganga alivua nguo zote na kuanza kuimba nyimbo za kilugha. Na tuliposogea hatua kulifikia, jiwe lililolifunika pango likafunguka, tukaingia.

Mle ndani kingo za pango zimechongwa mithili na kitu kama greda. Mle ndani nikaona fedha nyingi aina mbalimbali. Yule mganga akaniambia mle pangoni nitamuona rafiki yangu ambaye tulitoka wote Tanzania kuja kwa huyu mganga, tukapotezana kumbe yuko huku pangoni.

Akaniambia rafiki yako alikosea masharti. Sasa tulivyozidi kuingia pangoni, nikaona mwanga wa taa mbili zinawaka nikadhani ni taa. Mganga akaniambia una bahati wenzio huja huku na kukaa siku tatu hadi wiki bila kumuona mzee. Wewe umekuja leo tu na kumkuta.

Kisha akaniambia mkono wako una alama M. Hapo mwili ukasisimka nikaanza kujifikiria kwamba nikifa huku itakuwaje. Ndugu zangu hawataweza kuliona kaburi langu. Wakati nawaza, nikaona bonge la nyoka nikadhani ni tairi la trekta. Mganga akaimba wimbo wa mwisho, alipomaliza, nyoka akatoa ulimi. Mganga akaniambia nimsogelee mzee (nyoka) anataka kunisalimia kwa kunilamba mkono.

Mimi nikamwambia mganga naogopa hivyo naomba uniombee radhi juu ya hilo. Baada ya hapo mganga akaimba wimbo wa kuniombea msamaha. Kisha nyoka akajikunja na kurudi sehemu yake.

***Nini kiliendelea? Usikose sehemu ya mwisho. Una maoni, kisa? Ujumbe 0715268581***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Yaliyotokea kwenye sensa yatoe somo kuntu

TANGU kuanza kwa Sensa ya Watu na Makazi Agosti 23, mwaka huu, kumekuwa na taarifa nyingi ambazo zinaacha somo kubwa kwa Watanzania hasa watendaji wa serikali.

Hadi sasa, kazi inakwenda vizuri kwa maana ya kupata taarifa za mara kwa mara kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), ambazo zinaonyesha kazi inakwendaje na hadi sasa kaya ngapi zimefikiwa na makarani na idadi ya watu waliohesabiwa.

Aidha, Kamisaa wa Sensa, Spika mstaafu Anne Makinda, ameonekana maeneo mbalimbali nchini akihamasisha wananchi na kutoa ufafanuzi wa mambo kadha wa kadha ambayo ni muhimu kukamilisha kazi hiyo.

Kasoro zilizojitokeza ni baadhi ya makarani kutolipwa stahiki zao na wengine kupunjwa hali iliyoleta hofu. Hata hivyo, mara kadhaa viongozi akiwamo Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Alibina Chuwa, walifafanua kuwa fedha zilipelekwa kwenye halmashauri ambako ndiko walipaswa kuwalipa makarani hao kwa wakati.

Kadiri siku zinavyokwenda, malalamiko yanazidi kujitokeza na huku wengine wakisotea fedha zao kwenye ofisi za kata au vituo maalum. Jambo hili halistahili kwa kuwa linaathiri kazi kwa ujumla wake.

Pia baadhi ya wananchi wamekataa kuhesabiwa kwa sababu mbalimbali ambazo zikifuatiliwa kwa kina ni kwamba hawajaelimishwa vya kutosha kujua kinachofanywa na serikali na kwa kiasi gani kina umuhimu kwao. Lakini wengine ni kwa sababu wana malalamiko ya muda mrefu ambayo hayajatatuliwa.

Wilayani Babati kwa mfano, kuna mwenyekiti wa kitongoji amekataa kuhesabiwa yeye na wananchi wake hadi mgogoro wa ardhi uliodumu kwa muda mrefu utatuliwe. Hatua hiyo ilisababisha Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, kwenda kuzungumza nao ndipo wakakubali kuhesabiwa.

Mkoani Njombe pia kuna mwananchi amegoma kuhesabiwa hadi Mkuu wa Mkoa, Anthony Mtaka, alipokwenda kuzungumza naye akabadili uamuzi na kukubali kuhesabiwa. Hawa ni wachache walioandikwa na vyombo vya habari lakini kuna ambao wanawakataliwa makarani hadi wanalazimika kuondoka baada ya nguvu ya ushawishi kushindwa.

Hii inaonyesha bado kuna tatizo la uelewa kwa wananchi wengi na kazi kubwa ilipaswa kufanywa na wajumbe wa nyumba kumi na wenyeviti wa vitongoji na serikali za mitaa.

Naamini kama kungefanyika vikao kwenye vitongoji na mitaa kwa kushusha elimu ngazi hiyo, kwa kuwa na uwajibikaji mzuri kungesaidia sana wananchi kuelewa kinachozungumzwa na kama kuna matatizo yakafika kwenye mamlaka za juu mapema kabla ya siku husika.

Hii inaacha fundisho kwamba kunapokuwa na kampeni ya kitaifa mbinu za kutoa elimu ziwe kwa muundo tofauti tofauti, inaweza kuonekana ni wachache sana waliogomea zoezi hilo lakini kimsingi inaweka dosari.

Lililotia dosari kubwa ni makarani kutolipwa fedha zao au wengine kulipwa pungufu, yaani wamefyekwa fedha zao na watu ambao wameamua kufanya hivyo. Pia wako waliokwenda kufanya kazi kwa shingo upande kwa sababu kuna watu wamekula fedha zao. Jambo hilo si sawa kwa kuwa ni hujuma kwa kazi ya kitaifa, hivyo ni muhimu mamlaka zikafanya uchunguzi wa kina wa madai ya makarani ili kuchukua hatua.

Sensa inafanyika kila baada ya miaka 10 na inatumia fedha za Watanzania ambazo ni lazima kuwe na thamani ya fedha kwa kuwa kuliko kupoteza fedha hivyo zingeelekezwa kutatua changamoto zao za huduma muhimu za kijamii kama afya, elimu na maji.

Baadhi walisema hawaoni umuhimu wa kushiriki sensa kwa sababu wanaona hali zao za maisha hazibadiliki na wanaona fedha zinatumiwa ndivyo sivyo na baadhi ya viongozi wa serikali.

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), inaonyesha kila mwaka fedha zilivyotafunwa kwenye idara na ofisi mbalimbali za umma na wananchi wanaposikia hali zao zinazidi kuwa duni, wanaona hakuna umuhimu wa jambo fulani linapofanyika.

Hivyo ni lazima kuwe na uwajibikaji pande zote, wananchi wanapowajibika kufanyakazi na kulipa kodi, basi waliopewa dhamana nao watimize wajibu wao kwa kusimamia fedha ya umma ili ilete matokeo chanya kwa maisha ya wananchi.

Ni muhimu kuhakikisha kazi hazitolewi kwa kujuana kwamba unamjua nani au unajuana na nani au wewe ni mtoto wa nani ndio upate kazi husika, hilo likifanikiwa kutakuwa na uchaguzi wa watu wenye ujuzi sahihi kwenye majukumu yao.





Ilikuwa siku ya furaha kwa Angelina Leonard wakati alipofikisha siku yake ya kuzaliwa hivi karibuni na kuandaliwa sherehe ya aina yake jijini Dar es salaam









# MITINDO



# LAZIMA WAKUGANDE

MOJA ya mapambo yanayomfanya mwanamke kuwa na mvuto ni mavazi. Kama ataweza kupangilia vyema nguo, basi ni rahisi kupata marafiki kwa urahisi.

Kuna aina ya nguo ambazo mwanamke akivaa huwa na mvuto wa sumaku, huonekana mrembo na mwenye kung'aa zaidi.

Wataalamu wa mavazi wanasema nguo za kubana zinatosha kuwachanganya watu pale mwanamke anapozivaa.

Wanasema wanaume wanachopenda kwa wanawake ni sura ya msichana na mavazi pekee na ndio maana huwa hawaruki wakiona mwanamke kapendeza.

Ikiwa unajua jinsi ya kuifanya vizuri, basi kila mlango utagongwa kwako.

Unaweza kuwa na gauni refu au fupi inayobana mwili kiasi, au suruali na shati yenye kubana katika mitindo ya kisasa.

Mavazi haya yanakwenda sambamba na viatu vya kisasa kama vya visigino virefu, buti au sando zenye muundo wa kisasa.

Usiache kuweka vikorombwezo tofauti kunogesha zaidi, mfano cheni ya madini ya thamani, pete, saa maridadi na kuuweka uso kwa vipodozi laini.

URTEMBO

**Na Mary Geofrey**

# URTEMBO WA TATTOO

## Unogesha lakini madhara mengi





TATTOO ni urembo wa michoro unaowekwa juu ya ngozi ya binadamu kama ishara ya kuelezea hisia ya mtu kuhusu upendo, mapenzi na imani.

Urembo huu umeshika kasi miongoni mwa vijana hasa wasanii nyota wanawake kwa wanaume.

Hata hivyo, kuna kuna maoni tofauti kuhusu urembo wa tattoo, huku wataalamu wanaonya athari inayotakana na matumizi yake.

Licha ya maonyo hayo, wengi wanaona Tattoo sawa na urembo mwingine na hivyo wanashindana kubuni michoro mbalimbali ambayo mingine inashangaza watu.

Kuna baadhi wamegeuza michoro hiyo kama sehemu ya kuongeza hisia za wapenzi wao na hivyo hutumia pesa nyingi kwa ajili ya kubuni na kuchora.

Michoro inayoelezea hisia za mapenzi mara nyingi huwa inawaumiza wahusika, pale wawili hao wanapoachana na michoro hiyo kushindwa kufutwa kutokana na hatua ngumu za kuondoa.

Wataalamu wa urembo wanashauri kama mtu haoni umuhimu wa kuchora tattoo, basi aachane nayo kwani faida yake ni ndogo kuliko madhara.

MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# MIHOGO NA CHACHANDU



MIHOGO ya kukaanga ni chakula pendwa hasa ile inayoandaliwa kwenye vibanda.

Wengi wanavutiwa na aina hii ya chakula lakini baadhi hushindwa kula kwa sababu ya kohofia mazingira na wakati mwingine kutokana na umaarufu wao.

Leo tunaelekezana namna ya kuipika ili ule nyumbani kwako na familia yako kama vitafunwa, mlo kamili wa mchana au usiku.

**MAANDALIZI**

Mihogo mikubwa mitatu, mafuta lita moja, kitunguu kimoja, kitunguu swaumu kiasi, tangawizi kiasi, nyanya nne, limao moja, karoti nusu, hoho nusu, pilipili manga kidogo, chumvi na pilipili mbichi.

**JINSI YA KUANDAA**

Menya mihogo, ikatekate kiasi upendacho na kwa urahisi wa kuiva kisha isafishe, bandika karai, weka mafuta na mihogo ndani, kisha weka maji kidogo kisha funika na mfuniko unaozuia mvuke kutoka.

Mihogo ikianza kuchemka punguza moto iive taratibu na kulainika vizuri hadi maji uliyochanya na mafuta yakauke.

Kisha funua, utaona mihogo yako ikiwa imeiva vyema, acha kutoa mmoja mmoja ile ambayo imeiva na kuanza kukauka vyema, tayari kwa ajili ya kuliwa na kachumbari ama chachandu.

**CHACHANDU**

Osha nyanya, karoti, hoho, tangawizi, chukua sufuria uvisage uvitie, kisha katakata kitunguu tia, twanga pilipili uitie pia. Weka chumvi na pilipili manga.

Bandika jikoni uweke na maji nusu kikombe na unyunyuzie mafuta kiasi. Funika acha ichemke dakika tano, kisha kamulia limau uache ichemke kidogo, epua chachandu yetu itakuwa tayari kwa kuliwa na mihogo. HYPERLINK "https://drive.google.com/u/0/settings/storage?hl=en&utm_medium=web&utm_source=gmail&utm_campaign=storage_meter&utm_content=storage_normal" \t "_blank"

MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Usifanye makosa unapojenga nyumba ili kuepuka kuvuja

KUWA na nyumba bora na imara ni ndoto na furaha ya kila mtu anayemiliki au anayetarajia kumiliki nyumba hiyo.

Inapokuwa kinyume cha matarajio ya kumiliki nyumba ya vigezo hivyo, moyo huinama japokuwa wakati mwingine hali hiyo inasababishwa na kukosea uchaguzi wa wataalamu wa ujenzi wa nyumba husika ambao hujenga chini ya kiwango.

Mtaalamu wa masuala ya ujenzi, Abeid Ng`anzi, anazungumzia sababu mbalimbali zinazochangia baadhi ya nyumba kuvuja muda mfupi baada ya ujenzi wake.

Anasema ziko sababu mbalimbali zinazochangia nyumba nyingi kuvuja ambazo watu wanapaswa kuzifahamu na kuchukua hatua wanapojenga nyumba zao ili kuzuia athari kutokea baadaye.

Ng'anzi anataja miongoni mwa sababu kuu zinazochangia tatizo hilo kuwa ni pamoja na matumizi ya vifaa vya ujenzi vya hali ya chini ambavyo baadhi ya watu hufanya hivyo kwa kudhani kuwa wanaokoa pesa.

Sababu nyingine anasema baadhi ya vifaa vinavyovaliwa na mafundi wakati wa kuezeka huwa si rafiki kwa paa, hivyo kudhoofisha kifuniko cha paa ambacho baadaye hutengeneza ufa na kupitisha maji.

Mbali na sababu hizo, pia anasema paa la nyumba linaweza kuharibiwa na upepo kama halikuezekwa kwa utaalamu mzuri, hivyo kusababisha kuvuja.

Pia anasema muundo wa paa lenyewe pamoja na makosa yaliyofanywa wakati wa kuezeka ni sababu nyingine na kwamba kwa makosa hayo ya kuvuja kunaweza kutokea hata ndani ya mwaka mmoja baada ya ujenzi wa nyumba husika.

Nyingine anasema ni ufungaji mbaya wa paa wakati wa kuezeka na kwamba kasoro kama hiyo huonekana haraka ndani ya wiki chache baada ya nyumba kuanza kutumika.

"Paa linaweza kuvuja kwa sababu ya ukiukaji wa matumizi ya teknolojia ya ujenzi. Kwa mfano, kitaalamu unatakiwa kuweka nyenzo za kuezekea katika tabaka tatu, wewe unaweka tofauti na hapo na makosa mengine madogo yanayofanana na hayo yanayofanywa wakati wa kuezeka," anasema.

Ili kuepuka hayo, anashauri kwamba njia umakini unahitajika wakati wa kuchagua wataalamu wa kukuezekea, kutumia vifaa bora bila kujali gharama, kufuata kanuni zote za uwezekaji na kukagua paa la nyumba yako mara kwa mara angalau mara mbili kwa mwaka.

Pia anasema mmiliki wa nyumba anatakiwa kuondoa vitu vyote ambavyo hutuama juu yake ambavyo hutengeneza nyufa hususani vyuma na vitu vizito.



## Namna ya kuchagua madirisha ya PVC



KULINGANA na maisha ya kisasa, ujenzi wa nyumba na mapambo yake yamebadilika na kuwa ya kisasa zaidi.


Uwekaji wa madirisha ya plastiki maarufu kama PVC, ni sehemu ya mabadiliko hayo kiasi ambacho kuna ongezeko kubwa la watu wanaoweka madirisha hayo.

Hata hivyo, madirisha hayo yana faida kubwa katika kupendezesha nyumba na kuhimili vipindi vya hali ya hewa mwaka mzima.

Hizi ni baadhi tu ya dondoo muhimu ya kuchukua kabla ya kuweka madirisha ya PVC.

1: Lazima kufahamu idadi ya vyumba na gharama ya madirisha kila moja.
2: Hakikisha unajua upana na urefu wa madirisha ya nyumba ili kufahamu idadi ya PVC itakayotumika.
3: Hakikisha madirisha yanaweza kuhimili hali ya baridi na joto katika kipindi cha mwaka.
4: Nunu PVC kulingana na chapa za kampuni ambazo zinazalisha zenye ubora na imara.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
MUHIMU HAPA NI NAMBA ZAKO LAKINI KUKUMAKI SURA SIO RAHISI, MANAKE UKIPIGA MEKAPU UNAGEUKA MWARABU SITOKUJUA
NNAZO ZA NIDA
NALALAJE WAKATI NINA KISHIKWAMBI CHA SEREKALI NIME-KUJA KUUZIA SURA
SIJAKITAKA TU, NIKIKITAKA HATA UKESHE WIMA UTOKI NACHO
GESTI
NILIGOMA KUHESABIWA NIKAZANI NITABEMBELEZWA, AKAJA KALANI MSAIDIZI 'KANINYUKA NGUMI YA TAYA' NIKATOA USHIRIKIANO!
SAFI SANA
WE KONDA UNAMASWALI MENGI KAMA KALANI WA SENSA!...KWANI VIPI?
NAFANYA SENSA YA ABIRIA WANAOTAKA KUSAFIRI BURE,,,
NANI ASAFIRI BURE> KWANZA INAONYESHA HUJAHESABIWA KWA KULALA HUMU!
DUH!
UNANIRUDIA HAPA ASUBUHI HUO UKA-LANI WA SENSA TOKA LINI?
MIMI NI CHAGUO LA MWISHONI 'NAVOLUNTIA'
NAVOZUUNGUKA KUWASAKA MAKALANI WANIHESABU, UTAZANI MORISONI UWANJANI
SASA WAKIJA KUKUHESABU 'NIWAJIBUJE?'
WAWASHIE VIDEO, WAPE NA BIA ZIPO ZAKUTOSHA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
HATUKUBEBI UNAKIWEMBE MFUKONI...

# Russia yazidisha mashambulizi Ukraine

**LONDON,** UINGEREZA

WIZARA ya Ulinzi ya Uingereza imesema katika siku tano zilizopita, kuna uwezekano Russia kuzidisha mashambulizi yake katika eneo la Donetsk mashariki mwa Ukraine kwenye mkoa wa Donbas.

Jumamosi mamlaka ya kijeshi ya Ukraine ilieleza kuwa vikosi vyake viliwarejesha nyuma wanajeshi wa Russia katika maeneo ya Soledar, Zaitseve na Mayorsk katika mkoa wa Donetsk.

Katika hotuba yake kwa njia ya video juzi usiku, Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, alisema hali bado ni tete na ya hatari katika kituo cha nyuklia cha Zaporizhzhia kinachodhibitiwa na Russia.

Naye Rais wa zamani wa Russia, Dmitry Medvedev, ambaye ni mshirika mkuu wa Rais Vladimir Putin, alisema nchi yake haitasitisha harakati zake za kijeshi nchini Ukraine licha ya kutangaza rasmi kuachana na dhamira yake ya kujiunga na Jumuiya ya Kujihami ya NATO.

Wakati huo huo, raia wa Russia wanaoishi nje ya nchi wataruhusiwa kuomba pasipoti ya miaka mitano.

Hatua hiyo itakuwa tatizo kwa wale wanaohitaji pasipoti ya pili kwa sababu haitakuwa na chipu ya elektroniki.

Kuanzia juzi idara za kibalozi za Russia nje ya nchi zinasimamisha kwa muda kupokea maombi ya utoaji wa pasipoti halali kwa miaka 10, kulingana na tovuti ya Wizara ya Mambo ya Nje ya nchi hiyo.

Ujumbe huo ulionekana mapema kwenye tovuti za balozi katika nchi za Ulaya za Latvia, Estonia, Sweden, Italia, Ujerumani, Uturuki, Azerbaijan na Kazakhstan.

Aidha, viingilio vilivyoko tayari vya kuwasilisha nyaraka za pasipoti kwa njia ya kielektroniki vimefutwa.

Ijumaa, wafanyakazi wa BBC walipokea jumbe muhimu; moja kutoka idara ya ubalozi wa Latvia, nyingine Bosnia na Herzegovina.Wote wawili walitakiwa kujiandikisha kwa pasipoti ya miaka mitano.

Kwenye tovuti za balozi za Latvia na Uturuki, sheria hiyo mpya inaelezewa kuwa inatokana na sababu za kiufundi, na mwisho wake unasisitiza kuwa zitaendelea kutumika hadi suala la kutengeneza pasipoti na kibebea data cha elektroniki litakapotatuliwa.

Kutokana na hali hiyo, utaratibu mpya huenda umetokana na uhaba wa chipu kwa pasipoti za biometric.

Ukosefu wa vipengele dhidi ya historia ya vikwazo ilikuwa mojawapo ya sababu kuu kwa nini Wizara ya Maendeleo ya Dijiti ya Russia ilibidi kufungia mradi wa pasipoti za elektroniki, Forbes iliandika.

Olga Maklakshina, mkurugenzi mtendaji wa Sberbank, pia alizungumza juu ya ukosefu wa chipu kwenye kadi za plastiki.

Wafanyakazi walilazimika kutoa chipu kutoka kwa kadi za zamani na kuziingiza kwenye zile mpya.

BBC Idhaa ya Kirussia imewasiliana na Wizara ya Mambo ya Nje kupata ufafanuzi zaidi na inasubiri jibu.

**BBC**



Mwanajeshi wa Russia akilinda kinu cha nyuklia cha Zaporizhzhia ambacho ni kikubwa katika bara la Ulaya. **PICHA: AP**

## Mapigano yazuka Tripoli

**TRIPOLI,** LIBYA

MAPIGANO makali yamezuka katika mji mkuu wa Libya, Tripoli kati ya makundi yanayohasimiana kutokana na mzozo wa kisiasa kuhusu udhibiti wa nchi hiyo. Abdulmenam Salem, mkazi wa Tripoli alisema hali ni mbaya na hawakuweza kulala usiku kucha kutokana na milio yenye kutisha ya risasi na vilipuzi.

Picha na video za mapigano hayo zilirushwa mitandaoni, lakini shirika la habari la Reuters lilisema halikuweza kuzithibitisha mara moja taarifa hizo.

Ujumbe wa Umoja wa Mataifa nchini humo ulionya wiki hii dhidi ya jaribio lolote la kutatua mzozo huo kwa njia ya vurugu.

Mgogoro mkuu wa Libya ni kati ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa iliyoko mjini Tripoli chini ya Abdulhamid al-Dbeibah dhidi ya utawala pinzani wa Fathi Bashagha, unaoungwa mkono na Bunge la mashariki mwa nchi hiyo.

**DW**

## Papa Francis kuunda jopo la kumchagua mrithi wake

**ROME,** VATCAN

KIONGOZI Mkuu wa Kanisa Katoliki duniani, Papa Francis, jana alitarajiwa kuunda jopo la makardinali wapya 20 waliochaguliwa kutoka pembe nne za dunia, ambao wengi wao siku moja wanaweza kuishia kumchagua mrithi wake.

Papa Francis mwenye umri wa miaka 85 na aliyechaguliwa kuongoza kanisa hilo mwaka 2013, ameelezea uwezekano wa kustaafu kutokana na afya yake kuzorota, uamuzi uliochukuliwa pia na mtangulizi wake Papa Benedict wa 16.

Sherehe hiyo itafanyika katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Petro na itawajumuisha makasisi wanaojulikana kwa kazi zao za kichungaji, lakini maoni yao endelevu kwa Kanisa Katoliki lenye waumini bilioni 1.3 duniani kote.

Baada ya maaskofu 20 watakaotangazwa, Papa Francis atakuwa amewachagua makardinali 83 kati ya 132 ambao kwa sasa wana sifa ya kumchagua papa mpya.

**DW**

## UNICEF yalaani shambulizi shule ya chekechea Tigray

**NEWYORK,** MAREKANI

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la kuwahudumia Watoto (UNICEF), limelaani shambulizi la anga ambalo liliishambulia shule ya chekechea eneo la Tigray nchini Ethiopia.

Shambilizi hilo lilisababisha vifo vya watu wanne wakiwamo watoto wawili.

Tukio hilo limetokea juzi katika mji wa Mekele, siku chache baada ya kuzuka tena mapigano kati ya vikosi vya serikali ya Ethiopia na wapiganaji wa TPLF kwenye mpaka wa kusini wa eneo hilo.

Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Ayder iliyoko Mekele, Kibrom Gebreselassie, alisema watu wengine tisa wamejeruhiwa na wanapatiwa matibabu katika hospitali hiyo.

Vyombo vya habari vya Tigray vilisema idadi ya waliofariki imefikia saba, huku serikali ikiendelea kukanusha kukishambulia kituo cha watoto na kwamba waliyalenga maeneo ya kijeshi pekee.

**DW**

MAKALA

# TAASISI ZA MIKOPO PASUA KICHWA



Na Magabilo Masambu

Ni kweli kwamba kwa hali ya dunia ya leo hakuna anayeweza kuishi bila kuwa na fedha pamoja na kwamba fedha haiwezi kuwa suluhisho la kila jambo. Kuna matatizo mengine hata kama ungalikuwa na fedha kiasi gani, bado huwezi kuyatatua, kifo kikiwamo.

Lakini ukweli kwamba fedha ni muhimu sana katika maisha yetu ya kila siku unabaki pale pale. Kutokana na umuhimu huo, kila binadamu anahangaika kila siku ili kuipata fedha hiyo, ndiyo kusema kwamba njia za kuitafuta zinatofautiana katika wepesi au ugumu wake.

Leo nizungumze kuhusu wale wanaojipatia fedha kutoka taasisi za fedha kwa njia za mikopo. Kwanza, nakubaliana na mawazo ya wengi kwamba kama mtu hana kipato cha uhakika, ni vigumu kufanya maendeleo bila kuwa na mkopo. Lakini mikopo hiyo pia imegeuka kuwa chanzo cha umaskini na ufukara kwa walio wengi.

Ukitazama kwa haraka haraka, unaweza kudhani kwamba taasisi nyingi za mikopo zinakusudia kuwasaidia watu kumbe kinyume chake zinakusudia kutengeneza faida maradufu ili kujiendesha ikiwa ni pamoja na kulipa mishahara minono kwa watumishi wake.

Ukitaka kujua kwamba wanakusudia kutengeneza faida kwa namna zozote zile, utagundua kwamba hawa maofisa mikopo wanapokuja kwa mara ya kwanza kwa mteja, wanakuwa na lugha nzuri za kimalaika. Wanabembeleza kiasi cha kudhani kwamba wameshuka leo kutoka mbinguni. Ukishaingia wakakupatia fedha zao ukapangiwa siku ya kupeleka marejesho, hapo ndipo utaanza kuona rangi zao halisi, utafikiri umeingia magereza.

Kwa hiyo ni muhimu sana kwanza wananchi au wahitaji kuwa makini wakati wa kupokea taarifa na hasa juu ya makato kwa maana ya riba ambazo mara nyingi hawazielezi sawasawa zikaeleweka kirahisi. Kwa sababu hisabati pia ni tatizo kwa watu wengi, tumejikuta tukiingia mikataba ya ovyo bila kufahamu na unapoanza marejesho ndiyo unajua kuwa haikuwa kama ulivyoelewa. Pili, serikali ni muhimu sana kuzitupia macho baadhi ya taasisi ambazo zimekaa mtindo wa kikandamizaji. Uchumi wa mtu mmoja mmoja kwa serikali lisibakie kuwa jambo binafsi, bali taasisi hizi ziwe zinafuatiliwa. Natambua kwamba wengi watapata vibali baada ya serikali kupitia Benki Kuu (BoT) kuwapatia usajili wa kuendesha shughuli za kibenki, ambapo wengine huwa wanakuja kukiuka taratibu mbeleni katika utekelezaji wa shughuli zao.

Kwa kuwa Katiba inasema kazi mojawapo ya serikali ni kustawisha maisha ya wananchi wake, basi kulinda uchumi wao ili wasinyonywe na kuibiwa kwa kufirisiwa ni kazi ya serikali pamoja na wananchi wenyewe. Katika taasisi hizi, nadhani ziko ambazo zikikopesha huwa hazikusudii kurudishiwa fedha zao, bali zinakuwa zinalenga kuchukua zile dhamana za mkopo wenyewe. Nasema hivyo kwa sababu ziko taasisi za fedha ambazo zimelalamikiwa na zinajulikana kwamba ukikopa lazima wakufirisi.

Wananchi wanazijua na wao wanajijua, hivyo acheni hizo dhuluma. Unaweza kuona hakuna madhara ya kufanya uhuni huo, lakini mtatengeneza laana za familia zenu. Kama mnakusudia kuwasaidia watu, saidieni kwa nia njema ya kuwakwamua kiuchumi Watanzania wenzenu na si kukusudia kuchukua jasho lao.

Kwa upande wa wananchi, moja ni muhimu pia kuwa makini kwa taasisi zinazowafuata kwamba zina fursa za mikopo. Pili, kuwa na malengo ya kuzichukua fedha zenyewe na hasa kinamama. Kuna watu wanachukua mikopo wanakwenda kufanya sherehe mtaani wamjue yeye nani. Wengine wanachukua wanapeleka kwa waganga wa kienyeji na kadhalika, mwisho wa siku wanashindwa kurejesha na vitu vinauzwa.

Wako wengi waliopoteza maisha kwa mambo ya mikopo isiyo na msingi. Wengine wameishia kuwa wagonjwa wa presha, sukari, kupooza na kadhalika. Ukifuatilia utakuta wameshindwa kurejesha mikopo. Wako wanaochukua mikopo wenza wao bila kujua, wanaweka dhamana ya mali za nyumbani bila kuwekana wazi.

Mama anaweza kwenda kuchukua mkopo halafu mdhamini mumewe huku jamaa hana habari. Mwisho wa siku anashangaa tu timu inatinga pale nyumbani ohoo sisi ni maofisa mikopo kutoka Masambu Company tunahusika na utoaji wa mikopo! Jamaa akisikia tu hivyo na hajawahi kuchukua, kabla hajamaliza ameshaanguka chini kazimia. Mikopo mingine imevunja ndoa, wengine wamejiua na mambo kama hayo. Pamoja na tahadhari zinazotakiwa kuchukuliwa na mwananchi mmoja mmoja dhidi ya taasisi zenye nia ovu, serikali pia ina wajibu wa kuzifanyia mapitio ya kila wakati kuona zinaendeshaje shughuli zao.

Wanasema samaki mmoja akioza wote wameoza lakini kule Musoma samaki aliyebanikwa akioza tunamchomoa kisha tunamwanika juani, wadudu wanatoka tunamkaanga tena anakuwa kitoweo. Huwa hatutupi wote ndivyo ilivyo. Si kwamba taasisi zote ziko hivyo kwani baadhi zimewasaidia watu wanaochukua mikopo na kuitumia kwa malengo mazuri na wamefanikiwa katika biashara na kadhalika.

Mwisho, taasisi za fedha zisiwe zinaishia kutoa mikopo. Kama zinataka kupata wateja wa kudumu na taasisi ziwe imara, zina wajibu wa kuwapa elimu ya matumizi sahihi ya fedha zinazowakopesha wateja. Ikiwezekana pia biashara zao zizifahamu ili kuwasaidia na kama wanazalisha wazalishe sana ili kesho waongeze kiasi cha kukopa.

Kwa mantiki hiyo, taasisi hizo zisiishie kuwapatia fedha tu halafu kesho zinaingia laana ya kwenda kuchukua mali ambazo zingewasaidia hata watoto wakapata maisha yao. Kwa kufanyah ivyo zitaacha kuongeza umaskini na migogoro kwenye familia na serikali.Utajisikiaje kusikia mteja wako uliyemkopesha fedha amejinyonga kwa sababu ya fedha unazomdai? Hivi katika hali ya kawaida utakuwa na amani unapoendelea kukopesha wengine? Wasaidieni watu wajenge taasisi zenu ili kujitanua zaidi.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Sikinde, Vijana Jazz wanauliza, wivu ni sumu au kinga katika mapenzi? - 1



Na Adam Fungamwango

Wivu ni kumwonea mtu kijicho, kutotaka mwingine apate au kufanikiwa kwa sababu wewe hujafanikiwa kama yeye. Unataka uwe na kile ambacho mwenzako anacho, au hutaki mwenzako apate kitu chochote. Pia wivu ni husuda.

Wivu upo wa aina nyingi sana, ukiondoa huo, uko wa mapenzi. Wivu wa mapenzi unachukuliwa kama hisia kali ambazo mtu anazo juu ya mpenzi wake. Kutokana na kumpenda, kummiliki, hatotaka mtu mwingine yoyote kuingilia penzi lake.

Wakati mwingine inakwenda mbali zaidi kwani mtu anafanya wivu kwa hisia tu. Kuna wengine hawataki hata wenza wao wasalimiane na watu wengine. Hawataki wasafiri peke yao hata kuwaruhusu kwenda kwenye shughuli za kijamii au hata kufanya kazi.

Kuna wanaume ambao mkewe akichelewa hata kurudi dukani tu au sokoni ni matatizo. Ataulizwa na wakati mwingine kuadhibiwa. Wako wanaosema binadamu ni lazima awe na wivu kwa mpenzi wake. Bila wivu basi huyo aliye naye hampendi!

Kwa upande mwingine, wako wanaosema uko ule wa kawaida, kama binadamu na iwapo utathibitisha kile kinachokufanya uwe hivyo. Lakini wengi walipigwa wivu wa hisia. Huo ndio wivu mbaya sana. Ukichelewa nyumbani kosa, ukisalimiana na mtu matatizo.

Inafika wakati wanandoa au wapenzi wanakaguana kwenye simu kuyatafuta makosa. Huo ndio wivu wa hisia ambao msingi wake ni kutomwamini mwenzako na mara nyingi huumiza moyo na kusababisha ugomvi usiokwisha kwa kudhania kitu ambacho hakipo. Unakitafuta mwenyewe lakini hukioni.

Wenyewe wanasema mtu mzima na akili zake akikubali na akasema kama anakupenda na ukawa naye, akaacha wote na kuwa na wewe kwa shida na raha, au akaacha wengine na kukubali uwe mpenzi wake, amini hivyo tu. Mwamini kuwa anakupenda na anafahamu anachokifanya ukitaka umtendee kama mtoto mdogo hutafika naye mbali.

Wanasema wivu unatowesha amani na kuaminiana katika mahusiano. Unapokuwa na wivu unamfanya mwenzi wako akose uhuru wa kuongea na watu wengine kisa umeweka kwenye mazingira ya kumchunguza mwenzi wako. Inashangaza kuona watu hawaaminiani na kuwachunga wapenzi wao kama mifugo. Wanadai inawezekana ikawa ni hofu ya kumkosa mpenzi wako, lakini inabidi ujiulize kwa nini amekukubali wewe na si mtu mwingine?

Wanamuziki wa dansi miaka hiyo waliimba nyimbo mbalimbali hukusu wivu. Tuanze na DDC Mlimani Park Orchestra katikati ya miaka ya 1980. Walieleza jambo hilo na ulikuwa mzozo kati ya mume na mke. Mke anamjia juu mumewe ambaye ana wivu hadi anatoroka kazini na kumfuata nyuma nyuma anapokwenda dukani au sokoni kuangalia anasimama na nani. Wimbo unaitwa 'Wivu'.

"Baba watoto kaa nikueleze, siku hizi umebadilika, naona wivu umekuzidi na tena mimi huniamini. Nashangaa nimegundua, ukiwa kazini huishi kuaga na kuja kunichunguza nyumbani, ooo, baba watoto, oooo, niendapo sokoni au dukani unanifuata nyuma nyuma kuchunguza nimesimama na nani."

Mume naye anajitetea kuwa anafanya hivyo kutokana na kuambiwa maneno mengi na majirani.

"Siyo wivu mke wangu ee, naona uchungu kusikia, maneno kwa majirani, mimi nina wasiwasi."

Mke sasa anampa mumewe mbinu ya kukabiliana na jambo hilo na sivyo hivyo anavyofanya.

"Wasiwasi wako oo mume wangu, usikie ya kuambia mpaka uone mwenyewe."

Mume akakubali, lakini kwa shingo upande na anamwambia mkewe.

"Mhhh, kama ni wasiwasi haya, linalosemwa na watu mwisho wake huonekana."

Huu ni wimbo mmoja tu unaoonyesha kuwa mambo hayo yapo kwenye jamii yetu na yanaleta mtafaruku mkubwa. Vijana Jazz Band katikati ya miaka ya 1980 nao walikuja na wimbo wakauita 'Wivu'. Huu sasa mke anamwonea wivu mumewe ila kwa bahati nzuri mwenyewe anajijua ana wivu, lakini hawezi kujidhibiti.

"Wivu ee wivu ni ugonjwa jamani ee, wivu juu ya mume wangu utaniua, utanikondesha ee, hospitali ya wivu sijaijua ee mama ee, ningekwenda siku moja nikatibiwe, wasinisemesema wenzangu ooo mama ee, wananisengenya wenzangu mimi, naoha haya mama.

Akitoka asubuhi kwenda kazini sina raha, natamani niende naye mume wangu jamani, ninashinda mnyonge sina raha masikini, chakula sikitamani sina mama yoyo, kutwa natazama njia, atarudi saa ngapi, mapenzi mapenzi yamenipiga fimbo.

Aaaee mimi oo, jambo moja nawaomba ngoja niseme, acheni nifanye wivu kwa wangu kipenzi, bila wivu atajuaje kama kweli nampenda oo mimi. Kwenye moto pakitoka moshi kwenu kawaida, penye penzi pakitoka wivu mnashangaa, nawaomba mnielewe, mnielewe mimi, wivu ni kinga kweli ya mapenzi ee."

Mama analalamika kweli. Lakini mumewe akamkosoa.

"Wivu ukizidi unaleta kero mamaa, unaleta zogo bibi ee, hata nikienda kazini unaona wivu, unaonda donge, bibi ee, vipi 'darling?'

Baada ya kuambiwa hivyo mke akaleta hoja ambayo inamsababisha kutomwamini mumewe.

"Mbona saa zako za kurudi kazini hazieleweki mume wangu eee, mara saa kumi, mara saa mbili usiku nikueleweje, unanipa wasiwasi, mume wangu eee ninakonda ee."

Mume hakujibu ni kwa nini anarudi mida tofauti kama alivyoulizwa, ila kujulisha athari ambazo wanaweza kuzipata kama akindelea na wivu wake kuwa wanaweza kukosa pesa ya kununulia chakula na mavazi.

"Penzi lako linataka eti nishinde ndani tu, mama, tutakula nini, tunavaa nini, acha wivu ee."

Yalikuwa majibizano ya mume wa mke. Hayo ni mambo ya wivu. Je, ni sumu au kinga ya mapenzi? Tukutane sehemu ya pili Jumapili ijayo

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

PRINCE Petit kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja mmoja tu na walipomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile, badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoena na mtu yeyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane tu alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani Anapofika umri wa miaka 25, baba yake mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi. Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

# Mwisho wa Mauaji - 16

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

POLE sana mwanangu. Narudia tena kukupa pole. Kiufupi ni kwamba mimi nawafahamu wote uliowaua.

Nilikuwa nasikia vifo vyao, lakini nilikuwa sijajua sababu haswa, mara wengine kwa kupigwa risasi, wengine ajali ya gari, sikujua kama kuna hili unaloniambia. Ukweli mwanangu umeua watu muhimu sana kwenye maisha yako."

Hilo lilimshtua Prince. Kila hatua anayopiga inakuwa ngumu zaidi. Anataka kufahamu kama Hidaya ni mama yake mzazi. Lakini anaongezewa kwa kuambiwa aliowaua walikuwa watu muhimu sana kwake na kwenye maisha yake. "Kwa nini. Kwani kuna nini?" Akajiuliza mwenyewe.

Sura na macho yake yalionyesha kabisa kama ni mtu aliyechanganyikiwa na haelewi mambo yanakwendaje.

"Ina maana baba alikuwa ananidanganya?"

"Ndiyo, huyo baba yako kakuingiza mkenge. Uliowaondoa kwenye uso wa dunia ndiyo walikuwa msaada mkubwa kwako. Ulikuwa unajitumbukiza kisu mwenyewe tumboni. Hata mimi ni msaada kwako na ndiyo maana ilikuwa pia niuawe. Ashukuriwe Mungu umeniacha hai, tena kwa sababu ya Hasnat. Vinginevyo nisingekuwa hai. Na usingefahamu chochote kuhusu hili hadi unakuwa mzee na unakwenda kaburini."

"Sasa mama, baba anafanya hivyo kwa sababu gani na kwa manufaa ya nani? Mbona ananifanyia hivi mimi mtoto wake?" Prince akauliza tena.

"Usiwe na wasiwasi utajua kila kitu." Akasema na kumgeukia Hasnat. "Na wewe mchana huu sasa nenda kapike, watu njaa zishaanza kuwauma."

"Mmmh mama, mimi nasikiliza." Akajibu kwa kudeka huku akijikunjakunja.

"Haya mimi siongei kwanza, nenda kakatekate nyama ubandike, halafu uje."

"Haya." Akasema huku akiinuka na kwenda kufanya kile alichoagizwa, kuyatarisha chakula cha mchana.

Haikuwa rahisi. Kila mtu alikuwa anataka kujua nini kitaendelea. Hasnat alifanya alichoagizwa upesi upesi, halafu akarejea pale pale alipokuwa awali kusikiliza kile kilichokuwa kinazunguzwa.




**"Nyinyi wanangu ni wakubwa, mnajua baada ya hapo nini kiliendelea. Iligeuka, penzi likawa kati ya Martin na Hilda. Liliwakuta watu waliopendana kweli kweli kutoka moyoni na si mmoja kumpenda mwenzake, mwingine kufuata pesa au mali.**

"Leo kama hukutuunguzia mboga sijui, mwanangu Prince ajiandae tu kula maharage, maana..." Mama akawafanya Hasnat na Prince waangue vicheko, ingawa ilionekana kuwa wanacheka mdomoni, lakini moyoni kila mmoja alikuwa anamsubiri kwa hamu Hidaya nini atachoendelea kukisimulia.

"Mwanangu Prince, kwanza nikupe pole sana kwa maswahibu yote yaliyokupata, tangu ulipokuwa mdogo hadi leo hii. Kabla sijakufunulia ya moyoni ngoja nikupe hadithi hii kwa kifupi iliyotokeza zamani sana. Miaka mingi iliyopita.

Simon alikuwa na rafiki yake Martin. Hawa watu walikuwa na uwezo. Walimiliki majumba, magari na miradi mbalimbali. Waliheshimika sana hapa mjini.

Siku moja Simon alikwenda kwenye hoteli moja kupata chakula cha mchana. Alikutana na msichana mmoja mrembo aliyeitwa Hilda mmoja wa wahudumu hapo. Alikuwa mrembo wa haja wanangu nakwambieni."

"Kama Hasnat vile?" Prince akadakia. Mama akacheka. Hasnat mwenyewe akatabasamu."Kwa kuona kaopoa msichana mzuri, Simon akamwambia rafiki yake. Si unajua mambo ya kutaka kutambiana. Akamwambia rafiki yake Martin kuhusu jambo hilo na kumtaka aende naye kwenye hoteli akamthaminishe. Ni kweli Martin alichokiona hakuamini macho yake. Msichana alikuwa mzuri kweli tena tofauti na alivyofikiria awali.

Simon alimpa kila alichohitaji msichana yule. Atake nini asikipate. Lakini mapenzi ni mapenzi na pesa ni pesa wanangu. Pesa hulainisha tu pale kwenye mapenzi, lakini pesa haiwezi kuzalisha mapenzi. Hilda akili yake ikawa kwa rafiki wa mpenzi wake, Martin. Alimpenda tangu siku alipomuona kwa mara ya kwanza akiletwa na rafiki yake Simon.

Macho ya mapenzi yanajuana. Watu wakitazamana tu kila mmoja anajua kuna kitu. Martin alihisi kitu kwa Hilda. Mwanamke ndiyo kabisa, jicho alioangaliwa tu alijua Martin ana lake jambo.

Ni kweli hakutaka kufanya chochote kwa sababu ni mpenzi wa rafiki yake, na kitendo hicho kingeweza kuvunja urafiki na kuzaliwa uadui. Akajitahidi kupotezea. Siku zote macho yakiona moyo unapenda, moyo ukipenda subira hauna, na subira ikitoweka aibu na woga hukimbia.

Martin alishamhusudu Hilda. Hakuwa na subira tena, siku moja akaamua kwenda peke yake hotelini, wakati Simon akiwa amesafiri.

Ni siku ambayo Martin aliona Hilda amefurahi kuliko siku zote kuona amekuja peke yake. Martin hakutaka kuongea chochote pale kwa kuogopa macho ya watu kwa sababu wanafahamu kuwa Hilda ni mpenzi wa Simon, akamuachia namba shemeji yake ili wawasiliane baadaye."

Mpaka wakati huo Prince na Hasnat walikuwa kimya, wakimtazama kwa makini Hidaya aliyekuwa mithili ya watoto waliokuwa wakimsikiliza bibi yao akiwapigia hadithi.

"Nyinyi wanangu ni wakubwa, mnajua baada ya hapo nini kiliendelea. Iligeuka, penzi likawa kati ya Martin na Hilda. Liliwakuta watu waliopendana kweli kweli kutoka moyoni na si mmoja kumpenda mwenzake, mwingine kufuata pesa au mali.

Ni wakati huo huo, kabla hata hajafahamu kama amesalitiwa, Simon akapata matatizo, akakamatwa na kushtakiwa kwa makosa ya kununua mali ya magendo kwa ajili ya kuweka kwenye duka lake, akafungwa jela mwaka mmoja. Huku nyuma penzi likakolewa kiasi cha kuamua kufunga ndoa." Hidaya akasita na kutoa kikohozi chepesi.

"Alipotoka jela?" Hasnat akauliza haraka haraka.

"We nawe mbea weee, basi tu."

"Mhh, maana naona hadithi imekolea, imefika penyewe," binti akamjibu mama yake.

"Alitoka baada ya kukaa miezi minane. Alikuta ndoa imefungwa. Huwezi kufanya chochote wakati tayari watu wameshafunga ndoa. Tena kwa mtu ambaye hukuwa umemuoa, kumlipia mahari au kumchumbia. Ilibidi akubali matokeo. Aliwafuata na kuwaambia yeye hana kinyongo kwa sababu wanawake wako wengi na akampongeza rafiki yake akimwambia inawezekana kama asingemchukua yeye, basi angeweza kuchukuliwa na wanaume wengine wakati yupo jela. Hilo liliwatia moyo wanandoa."

Mhhh, ilitoka rohoni hiyo mama?" Akauliza Prince.

"Naendelea hivyo nisikilizeni. Miaka miwili baada ya ndoa Martin akapata ajali mkoani Morogoro alikokwenda kibiashara. Gari lake lilipinduka na kuanguka kwenye korongo moja kubwa, akapoteza maisha. Bahati nzuri mwili ulipatikana akazikwa kwa heshima. Hilda akabaki mjane masikini.

Baada maombolezo kumalizika na kila mmoja kurejea kwenye hali yake ya kawaida, Simon akamfuata Hilda na kumhitaji tena.

Alikataa, kwa sababu ya kulinda ndoa yake, lakini akambembeleza sana, akimkumbusha kuwa yeye ndiye aliyekuwa wa kwanza kuwa mpenzi wake kabla ya marehemu rafiki yake. Tena kwa kumnyang'anya tonge mdomoni. Akamuahidi atampenda na kumtunza kama rafiki yake. Akamuahidi pia kumuoa, kwa sababu bado Simon alikuwa hajaoa ingawa alikuwa na mahawara kibao."

**ITAENDELEA JUMAPILI**

# MUME WA NISHA APIGA MKWARA



BAADA ya kufunga ndoa mume wa Salma Jabu maarufu Nisha, amesema hatakuwa kizuizi cha mkewe kufanya kazi, lakini apate ruhusa kutoka kwake.

Salim amesema dini inataka mke akifanya jambo lolote ni lazima apate ruhusa ya mume, hivyo Nisha atafuata sheria hiyo na sio kumzuia kufanya kazi zake.

Kwa upande wa Nisha, amesema anajisikia furaha kuingia katika maisha ya ndoa na kwamba atahakikisha hali ya vicheko itaendelea ndani ya nyumba katika maisha yao yote.

“Nitamsikiliza mume wangu kile anachotaka, nimeingia katika maisha ya ndoa lazima nifuate misingi hiyo na nitajitahidi furaha hii idumu maisha yetu yote,” amesema.

# PrayGod, Godfrey wawasha moto kiaina

WAIMBAJI wa muziki wa Injili, PrayGod Sawe na Godfrey Steven wameendelea kuwapa raha wapenzi wa muziki huo kwa kolabo yao inayoitwa ‘Nimeridhika’.

Akiuzungumzia wimbo huo ambao tayari unafanya vizuri kwenye chati za gospo nchini, PrayGod amesema Mungu ameendelea kuwatumia kwa viwango vikubwa ili kufikisha ujumbe kwa jamii yote.

“Kwa kifupi tumewasha moto, wimbo umewabariki wengi na kama unavyojua sisi ni vijana lazima tumtumikie Mungu, wimbo tayari umetoka na unapatikana kwenye mitandao yote na chaneli yangu ya YouTube,” alisema PrayGod.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RONALDO KUTIMKIA NAPOLI
MWAKILISHI wa Cristiano Ronaldo, Jorge Mendes amezungumza na Napoli kuhusu uwezekano wa kumnunua mshambuliaji huyo wa Manchester United na Ureno mwenye umri wa miaka 37. ***(Sky Sports)***

### MAN KUTAFAKARI
KLABU ya Manchester United wanatafakari iwapo wataachana na harakati zao za kumnunua Antony baada ya Ajax kukataa ofa ya tatu ya pauni milioni 76 kwa mshambuliaji huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 22. ***(Telegraph)***

### FIRMINO KUMBADILI PAREDES
LIVERPOOL huenda wakamtoa mshambuliaji wa Brazil, Roberto Firmino mwenye umri wa miaka 30, ili kumpata kiungo wa kati wa Paris St-Germain na Argentina, Leandro Paredes mwenye umri wa miaka 28. ***(Calciomercato)***

### FOFANA SAFI CHELSEA
KLABU ya Chelsea wamefikia makubaliano ya kumsajili beki wa Leicester City, Wesley Fofana mwenye umri wa miaka 21, kwa ada inayoaminika kuwa pauni milioni 70. ***(The Athletic)***

### AKANJI KUMRITHI FOFANA
KLABU ya Leicester wanafikiria kumnunua kwa mkopo beki wa Borussia Dortmund na Uswisi, Manuel Akanji mwenye umri wa miaka 27, kama mbadala wa Wesley Fofana ambaye anatajwa kufikia makubaliano na Chelsea. ***(Mail)***

### ZAKHARYAN HUYO CHELSEA
CHELSEA wanakaribia kumsajili kiungo wa kati wa Urusi, Arsen Zakharyan mwenye umri wa miaka 19 kutoka Dynamo Moscow. ***(Mail)***

### AUBAMEYANG AKWAMA CHELSEA
JUHUDI za Chelsea kumnasa mshambuliaji wa Barcelona na Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang zimegonga mwamba kwa sababu ya kushindwa kufikia makubaliano ya maslahi binafsi huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 akitaka mkataba wa miaka miwili naoThe Blues wakijiandaa kumpatia mkataba wa mwaka mmoja pekee. ***(Sun)***

### KEANE ATAKIWA FOREST
KLABU ya Nottingham Forest imewasiliana na Everton kuhusu uwezekano wa kumsajili beki wa England, Michael Keane mwenye umri wa miaka 29 kwa mkopo. ***(Football Insider)***

### PAQUETA FRESH WEST HAM
KLABU ya West Ham imekubali dili ya kumnunua kiungo wa kati wa Lyon, Lucas Paqueta baada ya klabu hiyo ya Ufaransa kukataa ombi lao la kwanza la mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 24. ***(Sky Sports)***

### DIAZ AWANIWA VIGO
KLABU ya Celta Vigo imewasilisha ofa ya kumnunua mshambuliaji wa Blackburn Rovers na Chile anayenyatiwa na Everton, Ben Brereton Diaz mwenye umri wa miaka 23. ***(Football Insider)***

### O'RILEY AGONGANISHA TIMU
KIUNGO wa kati wa Celtic na Denmark mwenye umri wa miaka 21, Matt O'Riley anavutia hisia kutoka kwa Borussia Dortmund, Liverpool, Arsenal na Manchester United. ***(ESPN)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MAJERUHI SASA KUATHIRI MKATABA MPYA WA KANTE

### Kocha Thomas Tuchel asema pia umri na kiwango kitaangalia namna...

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel amefichua kwamba, historia ya hivi karibuni ya N'Golo Kante ya majeruhi bila shaka itazingatiwa katika mazungumzo ya kuongeza mkataba mpya wa kiungo huyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 amebakiza mwaka mmoja tu katika mkataba wake wa sasa hapo Stamford Bridge na The Blues wanataka kumbakisha huku London Magharibi.

Hata hivyo, Kante alicheza mechi 26 pekee za Ligi Kuu England msimu uliopita, idadi yake ya pili kuwa chini zaidi tangu atue nchini England mwaka 2015 na kwa sasa hayuko vizuri kutokana na tatizo la misuli.

Tuchel amekiri kwamba, msururu huu wa majeruhi wa hivi sasa utaathiri aina ya ofa ya mkataba ambayo Kante atapokea kutoka kwa Chelsea.

Alipoulizwa iwapo rekodi ya majeraha ya Kante inaweza kupuuzwa katika mazungumzo, Tuchel alijibu: "Huwezi. Unapaswa kuzingatia kila kitu kilichopo mezani na mezani ni uwezo wake, mezani ni ushawishi wake na ubora wake.

"Lakini kwenye meza, bila shaka ni umri wake, mshahara wake na kiwango chake cha majeruhi. Kutoka hapo unajenga picha nzima na kujaribu kutafuta suluhisho."

Kocha huyo raia wa Ujerumani alipoulizwa kama inawezekana kwa Chelsea kushinda taji kubwa zaidi bila Kante, alijibu: "Hili ni swali muhimu na jibu labda hapana, lakini tunajaribu.

"Ni ngumu zaidi kwa sababu unaona athari aliyonayo, unaona athari katika mabao ambayo tunafungwa, idadi ya mabao tunayofunga, idadi ya pointi tulizonazo, kiasi cha mabao anachotengeneza.

"Anatoa kitu cha kipekee sana na usisahau, pia anaweka imani ambayo huwezi kupima. Ndio maana yeye ni mchezaji muhimu. Lakini kwa wachezaji muhimu, ni muhimu sana kuwa uwanjani.

"Unaweza kuhesabu mechi ambazo amekosa, lakini vipi mechi mbili, tatu au nne za kwanza ambapo anahitaji kutafuta tena kiwango? Hakuna anayehesabu mechi hizi labda katika maisha halisi ni zaidi ya mechi alizozipata.

"Anarudi kwa mechi ya kwanza akitokea benchi na labda ya pili akitokea benchi, halafu ya tatu bado anahangaika kwa kujiamini na kucheza.

"Hii ndio hadithi na ndio, tuna matumaini makubwa tunaweza kubadilisha mambo, lakini huu ulikuwa mwanzo mbaya."


SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
PARIS ST GERMAIN
VERSUS
MONACO
1 | 1.22
X | 6.43
2 | 9.82

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KLOPP: LIVERPOOL INAHITAJI KIUNGO MPYA



**LIVERPOOL, England**

KOCHA Jurgen Klopp amekiri kuwa Liverpool wanataka kusajili kiungo wa kati katika siku za mwisho za dirisha la usajili la majira haya ya joto.

Kocha huyo raia wa Ujerumani amekuwa akisisitiza kwa muda mrefu kwamba, Wekundu hao wana namba za kutosha katika safu ya kati licha ya rekodi yao mbaya ya majeruhi.

Lakini sasa 90min ilifichua Ijumaa kuwa Liverpool wanataka kuingia sokoni kutafuta kiungo mpya, huku Konrad Laimer na Ruben Neves wakiwa miongoni mwa wale wanaowaniwa.

Na baada ya kuanza vibaya kwa msimu mpya ambao ulishuhudia wachezaji watatu wa safu ya kiungo, James Milner, Jordan Henderson na Harvey Elliott wakishindwa kufanya lolote wakati wakifungwa na Manchester United, Klopp ameibuka hadharani kuhusu hisia zake za awali.

Alipoulizwa kama anataka mchezaji mwingine kabla ya tarehe ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili, Klopp alijibu: "Hali hiyo itabadilika bila shaka.

"Najua tumekuwa na mjadala huu tangu yote yalipoanza na mimi ndiye niliyesema hatuhitaji kiungo, lakini nilikosea.

"Hiyo ndiyo hali. Kwa kweli hakuna la kusema zaidi kuhusu hilo. Tunatafuta, na kama ni mchezaji sahihi tunamhitaji na kama si mchezaji sahihi hatumhitaji."

Aliendelea: "Sijui (kama itatokea kabla ya Alhamisi), tutaona. Inahitajika kuwa mchezaji sahihi, lakini tunafanya kazi, na tutaona kama kitu kitatokea au la.

"Kama unavyoweza kufikiria, kwa kweli tunafanya kazi mara kwa mara juu ya aina hii ya mambo na kuna sababu kwa nini wakati mwingine haifanyiki, wakati mwingine ni ghali sana, wakati mwingine si mchezaji sahihi lakini basi hali inabadilika.

"Jambo moja linabaki kuwa muhimu na ni kwamba anahitajika kuwa mchezaji sahihi. Ikiwa tutafanya kitu itakuwa kwamba tuna uhakika kwa asilimia 100 kuhusu hilo na ikiwa hatujashawishika, basi hatufanyi. "

# Conte apanga kumpumzisha Kane

**LONDON, England**

KOCHA Mkuu wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte amekiri kwamba, atalazimika kuwapumzisha nyota wake wote katika kipindi cha wiki chache zijazo akiwamo mshambuliaji, Harry Kane.

Spurs wataanza msururu wa michezo saba kabla ya mapumziko ya kimataifa Septemba kwa safari ya kwenda Nottingham Forest leo Jumapili.

Kuanzia Oktoba hadi kuanza kwa Kombe la Dunia katikati ya Novemba, Tottenham itacheza mara 13 zaidi.

Mara nyingi Kane amekuwa akisisitiza kucheza kila mechi inapowezekana akiwa sawa na Spurs, lakini Conte amefichua kwamba wachezaji wake wote watahitaji kuondolewa kwenye kikosi cha kwanza katika kipindi fulani cha miezi michache ijayo.

"Narudia, tunazungumza juu ya hali ambayo tunapaswa kuanza kukabiliana nayo, Jumapili tunapaswa kucheza michezo saba kila baada ya siku tatu," Conte alisema.

"Baada ya kila mchezo, nitalazimika kuangalia hali ya wachezaji wote kwa uchovu na majeraha. Mchezaji mmoja kucheza katika michezo zote saba, haiwezekani.

"Mimi si mchawi! Siwezi kutabiri hili, lakini tunaenda mchezo baada ya mchezo kufanya maamuzi bora kwa timu na kwa wachezaji."

Tottenham wamesajili wachezaji sita kufikia sasa msimu huu wa joto, ingawa ni mchezaji mmoja tu kati ya hao alicheza muda wote mechi yake ya kwanza, Ivan Perisic dhidi ya Wolves, Jumamosi iliyopita.

Conte alisema hapo awali kwamba hii ilikuwa ni kujaribu kuegemea mwendelezo wa Spurs kutoka mwishoni mwa msimu uliopita, lakini wachezaji wake wengi wapya sasa wako tayari kuanza.

"Ni vyema kwangu kuwa na wachezaji mapema kwa sababu tunaweza kufanya kazi na wachezaji wapya na kuwaleta wachezaji hawa katika mawazo yetu," aliongeza.

"Richarlison, Clement Lenglet, Yves Bissouma, Ivan Perisic wako tayari kuingia kwenye timu na kucheza. Tutafanya hivyo kwa sababu itakuwa ni ujinga kufikiria tunaweza kucheza timu moja kila mechi ndani ya siku 23."

Y | CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# SPUTANZA YAPINGA WACHEZAJI KULAZIMISHWA KWA MKOPO

**Na Adam Fungamwango**

CHAMA cha Wachezaji wa Soka Nchini Tanzania (Sputanza) kimepinga hatua za baadhi ya klabu zinazotaka kuwatoa wachezaji wake kwa mkopo bila wao kukubali.

Mwenyekiti wa chama hicho, Mussa Kisoki, amesema ili klabu imtoe mchezaji kwa mkopo kwenda kwenye klabu nyingine ni lazima mwenyewe aridhie na kitendo cha kumlazimisha ni kosa.

Kisoki alisema hayo baada ya kuripotiwa kwenye vyombo vya habari kuwa klabu mbalimbali zinataraji kuwatoa wachezaji wao kwa mkopo kwenda kwenye klabu zingine ikiwa ni siku chache tu kabla ya dirisha kubwa la usajili kufungwa.

"Mchezaji ana haki ya kuhoji anakopelekwa, kule anakokwenda ni lazima ajue anaenda kuongeza kipaji chake au kuua, au anakwenda kuongeza kipato chake, au kitapungua, asiporidhia ni lazima ubaki naye au uvunje mkataba kwa kumlipa mishahara yake yote ya muda uliomsajili na fedha yake ya usajili," alisema Kisoki.

Alisema huenda kesi hizo zikawa nyingi baada ya dirisha la usajili kufungwa Agosti 31, mwaka huu.

"Nasikia kuna wachezaji wamegoma kuondoka kwenye klabu walizosajiliwa, kesi hizo zitakuwapo kwa sababu naambiwa wachezaji ni wengi waliogoma kuondoka kwenye klabu za Ligi Kuu," alisema Kisoki.

Mwenyekiti huo aliwashauri wachezaji wakatae kupelekwa kwenye timu nyingine kwa nguvu kama hawataki kwa sababu ni haki yao, ingawa kama wakikubali wenyewe basi hakuna tatizo.



Diwani wa Kata ya Kivukoni jijini Dar es Salaam, Sharik Shoghule (kushoto), akimvalisha skafu ya bendera ya Tanzania, Sri Sri Ravishankar Gurudev wa Taasisi ya The Art Of Living, aliyealikwa na Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo kwa ajili ya kueneza michezo mbalimbali hapa nchini. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ngao ya Jamii Zanzibar yasogezwa mbele

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), limesogeza mbele mchezo wa Ngao ya Jamii wa kuashiria kufungua rasmi pazia la Ligi Kuu ya Zanzibar msimu huu 2022-2023.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kamati ya Mashindano ya ZFF, mchezo huo umesogezwa hadi Jumatano ya Agosti 31, mwaka huu na utachezwa katika uwanja uliopangwa hapo awali wa Amaan majira ya saa 11:00 jioni.

Awali mchezo huo ulipangwa kuchezwa leo Jumapili ambapo utawakutanisha mabingwa wa Ligi Kuu ya Zanzibar, KMKM na mshindi wa Kombe la ZFF, wanajeshi wa Kipanga.

Akizungumza na gazeti hili Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano, Ali Bakari "Cheupe", alisema sababu kubwa ya kusogeza mchezo ni kupisha mchezo wa Timu ya Taifa ' Taifa Stars' dhidi ya Uganda katika michuano ya kufuzu kombe la CHAN.

Alisema wameona wawape fursa mashabiki na wadau wa soka visiwani Zanzibar kuangalia mchezo huo kwa utulivu ili kuipa hamasa timu ya Taifa.

Hata hivyo, mwenyekiti huyo aliwaomba radhi wadau wa soka Zanzibar kwa kuupeleka mbele mchezo huo na kuwataka kujitokeza kwa wingi Jumatano kuushuhudia mchezo huo.

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 28/08/2022


| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3933 | Dundee Utd vs Celtic | 15.11 | 7.25 | 1.15 |
| 14:00 | 4381 | Nantes vs Toulouse | 2.35 | 3.32 | 2.87 |
| 14:30 | 1148 | KAA Gent vs Royal Antwerp | 1.95 | 3.66 | 3.46 |
| 14:30 | 2567 | Hannover vs Greuther Furth | 2.16 | 3.45 | 3.05 |
| 14:30 | 3079 | Kaiserslautern vs Magdeburg | 1.91 | 3.84 | 3.39 |
| 14:30 | 4161 | Holstein Kiel vs Sandhausen | 2.04 | 3.60 | 3.20 |
| 15:00 | 2910 | Viborg FF vs Lyngby | 1.90 | 3.51 | 3.81 |
| 15:00 | 2953 | Randers vs Aalborg | 2.14 | 3.48 | 3.13 |
| 15:30 | 1205 | SBV Excelsior vs PSV Eindhoven | 8.22 | 6.01 | 1.26 |
| 15:30 | 3520 | FC Volendam vs Twente | 4.11 | 3.91 | 1.72 |
| 16:00 | 2768 | Brest vs Montpellier | 1.88 | 3.66 | 3.71 |
| 16:00 | 2899 | Aston Villa vs West Ham | 2.22 | 3.30 | 3.05 |
| 16:00 | 3302 | Lorient vs Clermont Foot | 2.04 | 3.32 | 3.52 |
| 16:00 | 4209 | Nice vs Marseille | 2.67 | 3.33 | 2.50 |
| 16:00 | 4233 | Troyes vs Angers | 2.48 | 3.22 | 2.77 |
| 16:00 | 4337 | Wolverhampton vs Newcastle | 2.65 | 3.15 | 2.60 |
| 16:30 | 4438 | FC Koln vs Stuttgart | 2.04 | 3.60 | 3.20 |
| 17:30 | 2155 | Torpedo Moscow vs FC Krasnodar | 3.30 | 3.40 | 2.07 |
| 17:30 | 2851 | Famalicao vs Santa Clara | 2.18 | 3.27 | 3.22 |
| 17:30 | 3258 | FC Winterthur vs BSC Young Boys | 4.82 | 4.22 | 1.59 |
| 17:30 | 4342 | FC Zurich vs FC Basel | 2.26 | 3.46 | 2.91 |
| 17:45 | 4454 | Cambuur vs AZ Alkmaar | 4.30 | 3.80 | 1.71 |
| 18:05 | 2387 | Reims vs Lyon | 4.11 | 3.91 | 1.74 |
| 18:30 | 2840 | Werder Bremen vs Eintracht Frankfurt | 2.44 | 3.50 | 2.60 |
| 18:30 | 2929 | Nottingham vs Tottenham | 6.19 | 4.39 | 1.45 |
| 18:30 | 3480 | Getafe vs Villarreal | 4.23 | 3.27 | 1.89 |
| 18:30 | 3794 | Racing Santander vs Real Oviedo | 2.75 | 3.00 | 2.60 |
| 19:00 | 3978 | Panetolikos vs Aris Salonica | 4.12 | 2.96 | 2.02 |
| 19:15 | 3928 | Kayserispor vs Giresunspor | 2.11 | 3.36 | 3.31 |
| 19:15 | 5097 | Kasimpasa vs Hatayspor | 1.99 | 3.52 | 3.47 |
| 19:30 | 1306 | Salernitana vs Sampdoria | 2.39 | 3.15 | 2.90 |
| 19:30 | 2314 | Verona vs Atalanta | 4.01 | 3.76 | 1.77 |
| 19:45 | 4029 | Rostov vs CSKA Moscow | 2.70 | 3.35 | 2.43 |
| 20:00 | 4458 | FC Arouca vs Sporting Braga | 4.71 | 3.71 | 1.69 |
| 20:30 | 1724 | Barcelona vs Valladolid | 1.19 | 6.53 | 13.24 |
| 20:30 | 2958 | Eibar vs Ponferradina | 1.75 | 3.49 | 4.48 |
| 21:00 | 3929 | OFI Crete vs Panathinaikos | 4.22 | 3.21 | 1.90 |
| 21:45 | 2245 | Parma vs Cosenza | 1.56 | 3.80 | 5.60 |
| 21:45 | 2384 | Pisa vs Genoa | 3.30 | 3.20 | 2.16 |
| 21:45 | 3407 | Trabzonspor vs Galatasaray | 2.23 | 3.32 | 3.07 |
| 21:45 | 3621 | Benevento vs Frosinone | 2.25 | 3.19 | 3.09 |
| 21:45 | 4181 | Perugia vs Bari | 2.37 | 3.15 | 2.95 |
| 21:45 | 4880 | Paris St Germain vs Monaco | 1.22 | 6.43 | 9.82 |
| 21:45 | 5185 | Cittadella vs Venezia | 2.22 | 3.20 | 3.15 |
| 21:45 | 5321 | Reggina vs Sudtirol | 1.96 | 3.35 | 3.70 |
| 21:45 | 5387 | Fiorentina vs Napoli | 3.09 | 3.49 | 2.13 |
| 21:45 | 5992 | Lecce vs Empoli | 2.31 | 3.36 | 2.86 |
| 22:30 | 5286 | Rio Ave vs Porto | 9.02 | 5.41 | 1.28 |
| 23:00 | 4659 | Espanyol vs Real Madrid | 6.05 | 4.64 | 1.45 |
| 23:00 | 5448 | UD Ibiza Eivissa vs Alaves | 2.91 | 3.16 | 2.39 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Agosti 28, 2022

Nipashe



**Majeruhi sasa kuathiri mkataba mpya wa Kante**

UKURASA 21



Mchezaji wa kikapu katika Sekondari ya High View, Mohamed Mafaty, akiruka juu kufunga goli, dhidi ya Sekondari ya Juhudi, wakati wa mashindano ya mpira wa kikapu kwa shule za sekondari yaliyofanyika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SIMBA SC YAKATAA KUMWACHIA ONYANGO

●●● Adaiwa kutaka kuvunja mkataba kwa kukosa namba, leo wanakiwasha Sudan dhidi ya Asante Kotoko na...

**Hadija Mngwai na Adam Fungamwango**

BAADA ya taarifa za beki wa kimataifa wa Simba, Joash Onyango raia wa Kenya kudaiwa kutaka kuvunja mkataba na klabu hiyo, uongozi wa klabu hiyo umesema kuwa bado unamwitaji mchezaji huyo katika michuano ya Kimataifa na Ligi Kuu Tanzania Bara.

Onyango ameripotiwa kutohitaji kuendelea katika klabu hiyo kutokana na kukosa nafasi katika kikosi cha kwanza baada ya kutua kwa beki kutoka nchini Ivory Coast, Mohammed Outtara aliyechukua nafasi yake.

Akizungumza na Nipashe, msemaji wa Simba, Ahamed Ally, amesema kuwa, beki huyo bado ana mkataba mbichi wa miaka miwili aliosaini baada ya kumaliza ule wa awali na kudai kuwa, bado anayo nafasi ya kupambana na kurudi kikosi cha kwanza.

"Joash bado ana mkataba mbichi wa miaka miwili aliosaini baada ya kumaliza mkataba wa awali, lakini yanakuja hayo ya kuvunja mkataba ni kutokana na kukosa nafasi katika kikosi cha kwanza baada ya kuja kwa Outtara," alisema Ally.

Aliongeza; "Lakini asikate tamaa ligi ndio kwanza inaanza, bado ana nafasi kubwa sana ya kuendelea kupambana na kurudi katika nafasi yake ya kikosi cha kwanza, hakuna asiyejua ubora na kiwango cha Joash.

"Nasema hivyo kwa kuwa tunafahamu tuna mashindano makubwa ya kimataifa mbele yetu na atatusaidia sana hata kwenye ligi ndio maana tulimpa mkataba mpya, bado ana nafasi kubwa sana ndani ya kikosi cha Simba, naamini atapata nafasi."

Wakati huo huo, kikosi cha Simba leo kinajitupa kwenye mji wa Khatoum nchini Sudan kucheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Asante Kotoko ya Ghana.

Mechi hiyo ni mfululizo wa michezo maalum iliyoandaliwa na wenyeji Al Hilal ya huko ambao wanaitumia kama sehemu ya kukiboresha kikosi chao chenye wachezaji wengi wapya kabla ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika mwezi ujao.

Simba iliondoka Ijumaa saa 10:00 alfajiri itacheza dhidi ya Asante Kotoko ambayo ilitwangwa mabao 5-0 na Al Hilal kwenye mechi ya kwanza ya michuano hiyo maalum. Kutokana na hali hiyo, Kotoko itataka kulipiza kisasi kwa Simba, huku Wekundu hao wa Msimbazi wakitaka kuwaonesha kuwa wao ni wakubwa kwenye michuano ya kimataifa.

Kocha Zolan Maki katika safari hiyo alisafiri na wachezaji 18, akiwakosa wachezaji tisa waliokuwa kwenye kikosi cha timu ya taifa pia Sadio Kanoute ambaye amekwenda kufuatilia pasipoti nchini kwao Mali, Joash Onyango ambaye inadaiwa kuwa amewasilisha barua ya kuomba kuvunja mkataba na Erasto Nyoni ambaye ni mgonjwa.

Baada ya mechi hiyo, Simba itajitupa tena uwanjani, Agosti 31 kucheza dhidi ya wenyeji Al Hilal, mechi ambayo inatarajiwa kuwa ngumu, haswa baada ya kutoa onyo kwa mabao 5-0 dhidi ya Asante Kotoko.

Simba inatarajia kukipiga na Nyasa Bullets ya Malawi, Septemba 9 ikianzia ugenini, wakati Al Hilal yenyewe inatarajiwa siku hiyo hiyo kuwa ugenini dhidi ya St George ya Ethiopia.

## Stars kazi kazi kwa Uganda leo

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars' leo inashuka dimbani kukabiliana na wapinzani wao Uganda katika mchezo wa raundi ya pili wa kuwania kufuzu michuano ya Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wanaocheza ligi ya ndani (CHAN). Mchezo huo utachezwa katika uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam. Stars itapambana kusaka ushindi katika mchezo huo wa kwanza ili kupata nafuu katika mchezo wa marudiano ambao utapigwa Septemba 3, mwaka huu katika dimba la St. Mary's, Uganda.

Kikosi cha Stars kinachonolewa na Kim Poulsen kinahitaji kupata matokeo mazuri katika uwanja wa nyumbani na ugenini kwa lengo la kupata nafasi ya kusonga mbele katika michuano hiyo.

Kuelekea katika mchezo wa leo Stars itawakosa wachezaji wawili kutokana na majeraha ambao ni Abdul Seleman 'Sopu' na Shomari Kapombe.

Akizungumza na gazeti hili jana, Poulsen alisema licha ya kukosa nyota hao wawili timu yake iko tayari kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri.

Alisema mchezo utakuwa mgumu kwa sababu Uganda wanacheza staili ya kushambulia zaidi na wamebaini ubora wa wapinzani wao na kuandaa mbinu za kiufundi.

**"Kwa maandalizi tuliyoyafanya tuko vizuri kwa ajili ya kuhakikisha tunapata matokeo mazuri, mashabiki wajitokeze kwa wingi kwa sababu tumejiandaa vizuri," alisema Poulsen.**

Nae golikipa, Aishi Manula alisema wamejiandaa vizuri kulingana na maelekezo ya benchi la ufundi na wanaenda kujitoa na kujituma kuhakikisha wanapata ushindi katika mchezo wa leo dhidi ya Uganda.

Mwisho.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >